**11 NOVEMBA, 2025**

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KWANZA

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 11 Novemba, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

### TANGAZO LA RAIS LA KUITISHA MKUTANO WA BUNGE

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:** Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba tutulie tuanze ratiba yetu. Ninaomba tutulie kidogo.

Waheshimiwa Wabunge Wateule, ninaomba nianze kwa kuwakaribisha Bungeni Dodoma. *(Makofi)*

Tunawapongeza sana kwa kushinda na kuchaguliwa kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Nikiwa Mtendaji Mkuu wa Mhimili huu pamoja na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, ninaomba kuwahakikishia ushirikiano mkubwa wakati wa kutekeleza majukumu yenu. Ninawahakikishia kwamba tutakuwa nanyi na tutahakikisha kuwa majukumu yenu ya Kibunge hayakwami na jukumu lenu la kuwawakilisha wananchi na kuisimamia Serikali yanafanyika ipasavyo. Karibuni sana, na sisi kama Ofisi ya Bunge tunajivunia kuwapokea. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama ambavyo *Order Paper* inabainisha, tutakuwa na shughuli kadhaa asubuhi hii na

nitaomba nianze kusoma Tangazo la Mheshimiwa Rais la Kuitisha Bunge. Tangazo hili ndilo ambalo linahalalisha uwepo wenu hapa na linatolewa kwa kuzingatia masharti ya Ibara ya 90(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tangazo la Mheshimiwa Rais linasomeka kama ifuatavyo: -

"Tangazo la Serikali Namba 647A la tarehe 4 Novemba, 2025 ambalo linahusu Hati ya kuitisha Mkutano wa Bunge iliyotolewa kwa mujibu wa Ibara ya 90(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

KWA KUWA, Uchaguzi Mkuu ulifanyika tarehe 29 Oktoba, 2025 katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977;

NA KWA KUWA, masharti ya Ibara ya 90(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inamtaka Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kuitisha Mkutano wa Bunge jipya kabla ya kupita siku saba tangu Tume Huru ya Uchaguzi kutangaza matokeo ya Uchaguzi Mkuu;

NA KWA KUWA, matokeo ya Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 29 Oktoba, 2025 yalikamilika kutangazwa na Tume ya Huru ya Taifa ya Uchaguzi katika majimbo yote ya uchaguzi tarehe 4 Novemba, 2025;

KWA HIYO BASI, mimi Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mamlaka niliyonayo chini ya Ibara ya 90(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ninaitisha Mkutano wa Bunge jipya la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ufanyike katika Ukumbi wa Bunge uliopo jijini Dodoma tarehe 11 Novemba, 2025 kuanzia saa 3.00 asubuhi.

Hati hii imethibitishwa kwa saini yangu na kuwekwa lakiri ya umma leo tarehe 4 Novemba, 2025."

Mwisho wa kunukuu, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba kuwathibitishia kuwa masharti ya Ibara ya 90(1) ya Katiba yamezingatiwa ipasavyo na Mkutano huu umeitishwa ipasavyo ndani ya siku saba tangu kukamilika kwa matokeo ya uchaguzi katika majimbo yote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea na hatua inayofuata na Mkutano huu sasa utajigeuza kuwa Kikao cha Uchaguzi wa Spika.

Waheshimiwa Wabunge Wateule, masharti ya Ibara ya 84(8) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yanasema kuwa wakati wowote Kiti cha Spika kinapokuwa wazi hakuna shughuli yoyote itakayotekelezwa katika Bunge isipokuwa uchaguzi wa Spika. Kwa kuzingatia kuwa kwa sasa Kiti cha Spika kiko wazi hivyo Bunge haliwezi kutekeleza shughuli yoyote mpaka limchague Spika.

Waheshimiwa Wabunge Wateule, Kanuni ya 9(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inasema mara baada ya kikao kujigeuza kuwa Mkutano wa Uchaguzi wa Spika, Katibu atamwomba Mbunge asiye mgombea wa nafasi ya Uspika kutoka miongoni mwa Wabunge ambao wamekuwa Wabunge kwa muda mrefu mfululizo kuwa Mwenyekiti wa Uchaguzi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kufanya uchambuzi kupitia Kumbukumbu za Ofisi ya Bunge, tumejiridhisha kuwa Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, Mbunge wa Jimbo la Ismani, Mkoani Iringa ambaye katika Bunge hili la Kumi na Tatu ndiye Mbunge wa muda mrefu aliyedumu tangu mwaka 1995 (miaka 30), anastahili kuwa Mwenyekiti wa kikao hiki cha uchaguzi wa Spika. *(Makofi)*

Hivyo, kwa heshima na taadhima ninaomba sasa nimlete kwenu Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi ili aongoze kikao hiki cha uchaguzi. *(Makofi)*

Mpambe mlete Mheshimiwa Lukuvi. *(Makofi)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. William V. Lukuvi) Alikalia Kiti*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge Wateule na Mheshimiwa Katibu wa Bunge, ninawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**WABUNGE FULANI:** Kazi iendelee.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Kwanza kabla sijaanza kazi yangu ninapenda nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sisi sote afya njema na kutuwezesha kuingia katika jengo hili. *(Makofi)*

Ninajua safari ilikuwa ndefu sana, kila chama kilikuwa na utaratibu wake, lakini wananchi wameamua sisi tuliopo humu ndani tunastahili kuingia hivi leo na kuanza kazi. Kwa hiyo, ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa niaba yenu kwa sababu ninajua hamna nafasi ya kusema. Tutakapoanza rasmi labda Mheshimiwa Spika atatoa salamu rasmi za Kibunge. *(Makofi)*

Pili na mimi ninawashukuru wapigakura wangu wa Jimbo la Ismani -Iringa kwa kuniwezesha kuingia humu ndani kwa kipindi cha saba tangu tumeanza mfumo wa vyama vingi mpaka leo. Kwa mara ya kwanza kipindi hiki cha saba nimepata kura nyingi kuliko vipindi vyote ambavyo nimewahi kutumikia, kwa hiyo, ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Ninajua sababu kubwa iliyonifanya nikapata kwa kweli, niseme wazi, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu hii ya Sita kwa sababu yale ambayo nilianza nayo tangu mwaka 1995 kuyaomba makubwa katika kila tarafa; Tarafa ya Idodi niliomba barabara ya kwenda *Ruaha National Park* na sasa inajengwa kilometa 104 kwa lami. Tarafa ya Ismani hatujawahi kuwa na maji ya bomba sasa yanatoka katika Awamu ya Sita. Tarafa ya Pawaga tuliomba mifereji ya kumwagilia maji kwa ajili ya kulima mpunga, sasa maji

yanatoka na mifereji inajengwa. Kutokana na haya, mimi ninajua ndiyo maana wananchi wameamua kunileta kwa kishindo. *(Makofi)*

Pia Mheshimiwa Rais amepata kura za kishindo kwenye Jimbo langu na amenishinda na mimi kwa sababu wanajua yeye ndiyo ameniwezesha. Sasa hadithi hii ninajua inawahusu wengi. Hadithi hii kwamba Mheshimiwa Rais katubeba inatuhusu tulio wengi humu ndani. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa niaba yenu ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutubeba. Kura zetu nyingi tulizozipata zimetokana na utendaji wa Serikali ya Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo machache ndugu zangu, ninawapongeza sana wote mlioshinda katika majimbo yenu na katika utaratibu mwingine na wale wa kuteuliwa, ninawapongeza sana sana.

Waheshimiwa Wabuneg Wateule, nipo hapa kusimamia uchaguzi, ingawa kulikuwa na uvumi kwamba nimegombea, ninataka niseme tu hapa kwa sababu nipo mezani, mimi sikugombea. Ninajua kwenye mitandao huko waliandika sana mimi nimegombea, mimi sikugombea na wala sikutamani kugombea. Mimi nilijua nitakuwa Spika wa kwanza hapa kabla Spika hajakanyaga kiti hiki, mimi nitakanyaga kwanza, nilijua hiyo nafasi nitapata lakini sikugombea nafasi ya Uspika, maana kwenye mitandao watu wamehangaika sana. *(Makofi)*

Basi baada ya hayo machache ndugu zangu, ninaomba nifanye kazi ya kikanuni iliyonileta hapa mbele. Kabla sijafanya nimwite..., kwa sababu bado hatujawa na Serikali kwa utaratibu wetu…

Baada ya maelezo yangu haya nitamwita Katibu wa Bunge atoe maelezo ya utaratibu wa uchaguzi halafu baadaye nitawaeleza hatua inayofuata.

Karibu Katibu.

## MAELEZO YA UCHAGUZI

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na kabla sijatoa maelezo ya uchaguzi ninaomba Waheshimiwa Wabunge Wateule mrejee Ibara ya 84(1) ya Katiba, ninaamini wote mna Katiba. Ibara ya 84(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini pia mrejee Kanuni ya 9 ya Kanuni za Kudumu za Bunge za 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada sasa ya kuomba Waheshimiwa wafanye rejea ya Ibara hiyo na Kanuni husika ninaomba sasa nitoe maelezo ya uchaguzi wa Spika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Ibara ya 84(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Spika wa Bunge anachaguliwa na Wabunge kutoka miongoni mwa Wabunge au watu wenye sifa za kuwa Wabunge. Aidha, Katiba inaelekeza kwamba uchaguzi wa Spika utafanyika wakati wowote katika Mkutano wa Kwanza wa Bunge jipya na katika Kikao cha Kwanza chochote mara baada ya Kiti cha Spika kuwa wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukidhi masharti ya Katiba niliyoainisha hapo juu, tarehe 4 Novemba, 2025 nilitoa Tangazo Namba 14824A katika Gazeti la Serikali Toleo Maalum Namba 11 kuutangazia umma kuwa Kiti cha Spika kitakuwa wazi kuanzia tarehe 11 Novemba, 2025 Bunge litakapokutana kwa mara ya kwanza baada ya Uchaguzi Mkuu na kwamba uchaguzi wa Spika utafanyika siku hiyo. Aidha, niliviarifu vyama hivyo kuwa chama chochote cha siasa chenye usajili wa kudumu kinachokusudia kusimamisha mgombea katika uchaguzi huo kiwasilishe jina la mgombea huyo ofisini kwa Katibu wa Bunge Dodoma kabla ya saa 10 jioni ya tarehe 10 Novemba, 2025 ambayo ndiyo siku ya uteuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niliwatangazia kuwa chama kinachokusudia kusimamisha mgombea ambaye siyo Mbunge kiwasilishe jina la mgombea huyo kwenye Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ili Tume ithibitishe iwapo mgombea huyo ana sifa za kuwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kulitaarifu Bunge hili Tukufu kuwa hadi kufika saa 10.00 jioni ya tarehe 10 Novemba, 2025 nilikuwa nimepokea majina yafuatayo ya wagombea: -

(i) Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu kutoka Chama Cha Mapinduzi; *(Makofi)*
(ii) Ndugu Veronica Charles Tyeah kutoka Chama cha *National Reconstruction Alliance (NRA);*
(iii) Ndugu Anitha Khalfan Mgaya kutoka Chama cha *National League for Democracy (NLD);*
(iv) Ndugu Chrisant Nyakitita Ndege kutoka Chama cha *Democratic Party (DP);*
(v) Ndugu Ndonge Said Ndonge kutoka Chama cha *Alliance for Africa Farms Party (AFP);* na
(vi) Ndugu Amin Alfred Yango kutoka Chama cha *Alliance for Democratic Change (ADC)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu utakaofuata sasa ni kwamba wagombea watafika mbele ya Bunge ili kujieleza kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza, kuulizwa na kujibu maswali matatu kama yatakuwepo na kisha kuomba kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuthibitisha kuwa wagombea wote wapo na wapo tayari kufika hapa. Baada ya zoezi la kuomba kura kukamilika kila Mbunge atapewa karatasi ya kura yenye majina ya wagombea na atatakiwa kupiga kura kwa kuweka alama ya vema katika mraba pembeni mwa jina la mgombea anayemtaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kura zitakuwa za siri ambapo kila Mheshimiwa Mbunge atapiga kura yake mahali alipoketi na baada ya hapo masanduku ya kura yataletwa mbele yakiwa wazi ili ninyi Waheshimiwa Wabunge kama wapigakura muweze kuyathibitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa kabla ya shughuli ya uchaguzi kumalizika Mheshimiwa Mbunge atakosea kuweka alama kwenye karatasi ya kura, ataruhusiwa kumrudishia Katibu karatasi hiyo na hapo hapo Katibu ataifuta na kuiharibu na kisha kumpa

Mheshimiwa Mbunge huyo karatasi nyingine ya kura. Baada ya hapo masanduku hayo ya kura yatapelekwa kwenye chumba maalum na kura hizo zitahesabiwa chini ya usimamizi wa wawakilishi walioteuliwa na wagombea mmoja kwa kila mgombea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo yangu, kama msimamizi wa uchaguzi, sasa naomba kukukaribisha ili uongoze zoezi la mgombea kujieleza na kuomba kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Kabla hatujaendelea, kwa utamaduni wa Bunge kwa sababu leo hatuna Serikali humu ndani, wananchi ambao siyo Wabunge huwa hawaruhusiwi kuingia humu mpaka kwa idhini yenu. Ndiyo utaratibu wetu, tumezoea hivyo kwa kanuni kwa hiyo, namuomba mtu mmoja wa Serikali aliyepo hapa ndani, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, atoe neno la kuwawezesha wenzetu hawa kuingia.

Karibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

**MHE. HAMZA SAIDI JOHARI – MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maelezo ya hoja ya kutengua Kanuni za Bunge kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 177(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025.

Kwa kuwa, Ibara ya 84(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inaweka masharti ya uwepo wa Spika, na kwamba atachaguliwa na Wabunge kutoka miongoni mwa watu ambao ni Wabunge au mtu mwenye sifa za kuwa Mbunge.

Na kwa kuwa, Bunge la Kumi na Tatu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linakusudia kumchagua Spika wa Bunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 9 ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Na kwa kuwa, miongoni mwa wagombea wa nafasi ya Uspika siyo Wabunge, na ili washiriki katika uchaguzi huo inabidi

waweze kuingia Bungeni kwa madhumuni ya kushiriki uchaguzi wa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Na kwa kuwa, Kanuni ya 163 ya Kanuni za Kudumu za Bunge inaweka utaratibu maalum kwa Wabunge, watumishi na wageni kukaa kwenye ukumbi wa Bunge.

Kwa hiyo basi, kwa mujibu wa Kanuni ya 177(1), naomba kutoa hoja ya kutengua Kanuni ya 163 ya Kanuni za Kudumu za Bunge ili kuwaruhusu wagombea wa nafasi ya Uspika, Ndugu Veronica Charles Tyeah kutoka Chama cha *National Reconstruction Alliance (NRA),* Ndugu Anitha Khalfan Mgaya kutoka Chama cha *National League for Democracy (NLD),* Ndugu Chrisant Nyakitita Ndege kutoka Chama cha *Democratic Party (DP),* Ndugu Ndonge Said Ndonge kutoka Chama cha *Alliance for Africa Farm's Party (AAFP)* na Ndugu Amin Alfred Yango kutoka Chama cha *Alliance for Democratic Change (ADC)* ambao siyo Wabunge waweze kuingia kwenye ukumbi wa Bunge kushiriki uchaguzi wa Spika wa Bunge la Kumi na Tatu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA - MBUNGE MTEULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Akhsante sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali, mnaweza kuketi Waheshimiwa Wabunge.

Sasa idhini ya kuingia itatolewa na Kiti kwa mmoja mmoja zamu yake ya kujieleza ikifika. Kwa sasa naomba wakae nje, wagombea wote na mgombea wa Chama Cha Mapinduzi Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu. Najua ni Mbunge miongoni mwetu, kwa hatua hii ninamuomba aende nje ili aungane na wenzake. Atarudi hapa wakati wa kupiga kura. *(Makofi)*

Sasa labda nikumbushe utaratibu wa kawaida tu wa chaguzi zetu, wakati wa hatua ya kwanza ya kujieleza ambayo haikuandikwa hapa, lakini tumezoea inapendeza zaidi tukiwasikiliza vizuri kila mgombea bila minong'ono wala kushangilia. Halafu kila mmoja tumpe nafasi yake tumsikilize, baada ya hapo uamuzi utakuwa wa kwako wewe kwenye karatasi. Mnaonaje hilo?

Eeh! Tusishangilie, tusicheke, tusipige makofi, wajieleze, watarudi nje, halafu mimi nitawaita mwishoni wakati tukishamaliza kupiga kura ili waweze kuteua mawakala wao. Kwa hiyo, kwa sasa tunaanza zoezi la uchaguzi.

Kama alivyosema Katibu wa Bunge, kila mgombea ataitwa hapa mbele yenu, atajieleza, nadhani ni dakika zisizozidi tatu. Kwa utamaduni wetu maswali hayazidi matatu, sijui Waheshimiwa Wabunge kama tunaelewana hapa.

Kwa utamaduni wetu na kanuni tumezoea maswali yasiyozidi matatu, kama hayapo nitamruhusu aende. Kwa hiyo wote watasikilizwa, hakuna mtu atakayepata bahati ya kumsikiliza mwenzake, atajieleza atatoka nje, halafu yule ambaye ni mbunge nitamuita wakati wa kupiga kura. Kwa hiyo, kwa kuanzia, leo tunao wagombea sita, kama alivyowatangaza. Kwa hiyo, mimi naanza kusoma kwa kadri walivyowasilisha barua zao hapa kwa Katibu wa Bunge.

Aingie Ndugu Veronica Charles Tyeah kutoka Chama cha *National Reconstruction Alliance (NRA)*. Barua yake ndiyo ilikuwa ya kwanza huyu, naomba mumuingize humu ndani.

*(Hapa Ndugu Veronica Charles Tyeah - Mgombea kutoka Chama cha NRA aliingia Ukumbini)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Tumesema msishangilie, *please*.

Ndugu Veronica Charles Tyeah kutoka Chama cha *NRA*, mbele yako, ndani ya ukumbi huu ni Waheshimiwa Wabunge.

Wako tayari kukusikiliza kwa maelezo utakayoyatoa na bila shaka umekuja kuomba kura.

Unapewa dakika tatu kujieleza na endapo ikiwapendeza Waheshimiwa hawa wanaweza wakakuuliza maswali yasiyozidi matatu. Ndugu Veronica karibu.

**NDG. VERONICA CHARLES TYEAH – MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA NRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunipa nafasi hii ya kusimama katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Waheshimiwa Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bwana Yesu Asifiwe.

**WABUNGE FULANI:** Amen.

**NDG. VERONICA CHARLES TYEAH – MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA NRA:** Tumsifu Yesu Kristo.

**WABUNGE FULANI:** Milele Amina.

**NDG. VERONICA CHARLES TYEAH – MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA NRA:** *Asalaam Aleykum.*

**WABUNGE FULANI:** *Aleykum salaam.*

**NDG. VERONICA CHARLES TYEAH – MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA NRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kujitambulisha majina yangu, ingawa Mheshimiwa Mwenyekiti amenitambulisha.

Mimi ninaitwa Veronica Charles Tyeah, ni mgombea wa Kiti hiki cha Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini pia nimeambatana na wageni wangu ambao ni Katibu Mkuu wa Chama cha *NRA* pamoja na Dada Jackline ambaye

niligombea naye nafasi ya Ubunge katika Chama cha *NRA*, yeye aligombea Jimbo la Ilongero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kusema lililonisibu na kuona kwamba ninafaa kugombea Kiti hiki cha Spika wa Bunge. Nitakapopata nafasi ama nitakapoteuliwa kuwa Spika wa Bunge, nina mambo makuu matatu ambayo natakiwa kuyafanya kama Spika wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele changu cha kwanza nitahakikisha kwamba ninaliweka Bunge katika usawa na Bunge hili liwe ni Bunge la wananchi na liwe lenye sauti ya kusikilizwa na wananchi, ili kuweza kuleta mabadiliko chanya katika Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba mbili; nitatamani kutoa Kambi Rasmi ya Upinzani na kuweka Kambi Rasmi ya Majadiliano ili majadiliano haya yawe na tija na kubadilisha Taifa letu na kuliweka katika umoja na mshikamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini namba tatu, ninatamani, nitakapopata nafasi ya kuwa Spika wa Bunge nitatumia *slogan* inayosema; "Taifa Kwanza Vyama Baadaye" nikimaanisha kwamba *slogan* hii imebeba ujumbe mzito sana. Endapo tutaitumia, tutakuwa mfano wa kuigwa kwa sababu imebeba ujumbe mzito. Tukitanguliza Taifa tukaacha tofauti za vyama, tutajenga Taifa lenye usawa na bora kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Ahsante sana Ndugu Veronica. Nakupa nusu dakika uombe kura.

**NDG. VERONICA CHARLES TYEAH – MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA NRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na samahani kama nitaenda tofauti na utaratibu, lakini nilisahau kupongeza Bunge hili kwa kuteuliwa na wananchi, lakini pia nampongeza Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ambaye amekuwa ni *role model* wa wanawake, amechaguliwa kwa kura nyingi na za kishindo. Hivyo mimi

Veronica amenipa nguvu za kusimama mahali hapa na kujiona kwamba ninaweza.

Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninaomba mniamini, naombeni kura zenu. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Ahsante sana Ndugu Veronica. Sasa ni zamu yenu Waheshimiwa Wabunge, kama kuna mtu mwenye swali aulize, anyooshe mkono.

Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro, alaa, unanyoosha mkono tu? Hakuna swali eeh?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** La pili?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** La tatu?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Ahsante sana Ndugu Veronica kwa maelezo yako. Unaweza ukatoka nje tumuite mtu mwingine. *(Makofi)*

Haya, aandaliwe Ndugu Anitha Khalfan Mgaya kutoka Chama cha *NLD*. Ndugu Anitha Khalfan Mgaya kutoka *NLD*.

*(Hapa Ndugu Anitha Khalfan Mgaya – Mgombea kutoka Chama cha NLD aliingia Ukumbini)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Ndugu Anitha Khalfan Mgaya**,** Mgombea Uspika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka *NLD,* karibu katika Ukumbi wa Bunge na mbele yako ni Waheshimiwa Wabunge hawa, wanasubiri kusikiliza maelezo yako yasiyozidi dakika tatu, lakini pia ikiwapendeza

wanaweza wakauliza maswali matatu. Kwa hiyo, karibu kwa maelezo.

**NDG. ANITHA KHALFAN MGAYA – MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA NLD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**WABUNGE FULANI:** Kazi iendelee.

**NDG. ANITHA KHALFAN MGAYA – MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA NLD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majina naitwa Anitha Khalfan Mgaya, nagombea nafasi ya Uspika wa Bunge kupitia chama changu cha *NLD*. Nipo hapa mbele yenu naomba kura zenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu yangu mimi ni mteknolojia wa maabara. Nilipata nafasi ya kugombea Ubunge kwenye Jimbo la Kibiti, nilipata kura nyingi sana, lakini hazikuweza kujitosheleza kuwa mmoja wenu leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo lengo langu la kuwa hapa mbele yenu ni kuomba kura zenu kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nikiwa na lengo kuu la kujenga mshikamano na maelewano katika nchi yetu hii ya Tanzania ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo mkinipa dhamana hii, endapo mkinichagua, nitahakikisha nasimamia misingi, sheria, haki, usawa, ufanisi na uwajibikaji wa kila mmoja wetu, lakini pia nitasimamia nidhamu, heshima katika kujenga hoja zetu na katika mijadala yetu. Endapo mkinichagua, kwa vile mimi ni kijana, nitawahimiza, nitawaelekeza vijana wenzangu jinsi gani ya kutunza amani katika nchi yetu maana amani, upendo na utulivu ndiyo tunu ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mkinichagua kuwa Spika nitahakikisha tunalisaidia Taifa huku tukishirikiana na Serikali yetu na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Waheshimiwa Wabunge, kwa unyenyekevu mkuu naomba kura zenu. Ahsanteni kwa kunisikiliza.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Ahsante sana Ndugu Anitha Khalfan Mgaya kwa maelezo. Sasa Waheshimiwa Wabunge, kama kuna mtu ana swali, swali la kwanza?

Mheshimiwa Esther, ni fursa ya kila mtu kuuliza swali eeh, siyo ajabu. Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO – MBUNGE MTEULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali kwa ndugu yetu Anitha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali dogo tu, katika maelezo yako umesema ni kati ya Wabunge ambao mmegombea kuomba ridhaa ya wananchi kuja Bungeni. Natambua tuna aina tano za makundi ya Wabunge ambao wanakuja kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Napenda walau unitajie aina za makundi manne tu kwa sababu unataka kuwa Spika wetu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Ndugu Anitha, ungependa kulijibu swali hilo?

**NDG. ANITHA KHALFAN MGAYA – MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA NLD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Nimempa fursa kwa sababu najua yeye amekuja kuomba hapa, anajua amekuja kuomba kura kwa Waheshimiwa Wabunge ambao wote ni Wabunge bila matabaka, mkishaingia humu wote ni Wabunge. Njia za kuingilia humu ziko nyingi, lakini ukishaingia huku ni Mbunge kwa hiyo, Ndugu Anitha tunakuruhusu, hakuna maswali mengine.

**MHE. HUSSEN N. AMAR – MBUNGE MTEULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana. Kuna swali.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** EEh! kuna swali lingine?

**MHE. HUSSEN N. AMAR – MBUNGE MTEULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Nani?

**MHE. HUSSEN N. AMAR – MBUNGE MTEULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa, hapa, hapa, huku.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Asimame huyo anayeuliza swali.

**MHE. HUSSEN N. AMAR – MBUNGE MTEULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Anha! Sheikh, karibu.

**MHE. HUSSEN N. AMAR – MBUNGE MTEULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo.

Kwa kuwa amesema tutakapompa ridhaa ya kuwa Spika atawaunganisha vijana wakati humu ndani kuna rika la wazee, je, anatuweka kwenye fungu gani atakapowaunganisha vijana? *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Ndugu Anitha, umemsikia vizuri?

**NDG. ANITHA KHALFAN MGAYA – MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA NLD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nimemsikia.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Unaweza ukasema kidogo?

**NDG. ANITHA KHALFAN MGAYA – MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA NLD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Haya ruhusa.

**NDG. ANITHA KHALFAN MGAYA – MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA NLD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema kwamba nitahakikisha ninawaeleza vijana, kulingana na uhalifu uliotokea, nitahakikisha ninawaeleza vijana kuwa Tanzania yetu inahitaji upendo, amani na furaha ili iweze kutimiza majukumu yake ya kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukiwa hakuna amani, upendo, furaha na tukizingatia vijana ndiyo nguvukazi, watashindwa ama tutashindwa kutekeleza majukumu yetu ya kitaifa. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Haya, ndugu Anitha, nadhani maswali yameisha, ninakuruhusu na ahsante sana kwa maelezo.

**MBUNGE FULANI:** Mwacheni shemeji yenu atoke. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa wagombea wanapoingia na kutoka wanawafurahisha sana, basi si vibaya wanapoingia na kutoka mnaweza kuwashangilia, maana naona mnafurahi sana mkiwaona wanatoka na kuingia, ila wakijieleza hapa kushangilia hapana, lakini mkifurahishwa na wanavyoingia na kutoka ni ruhusa kuwashangilia. *(Kicheko)*

Haya, anayekuja mgombea wa tatu ni Ndugu Chrisant Nyakititi Ndege kutoka *Democratic Party (DP)*. *(Makofi)*

*(Hapa Ndugu Chrisant Nyakitita Ndege – Mgombea kutoka Chama cha DP aliingia Ukumbini)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Ndugu Chrisant Nyakitita Ndege, kutoka Chama cha *Democratic Party,* karibu kwenye ukumbi wa Bunge.

**NDG. CHRISANT NYAKITITA NDEGE – MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA DP:** Ahsante.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Mbele yako humu ndani ni Waheshimiwa Wabunge, tunajua umegombea nafasi ya Uspika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hiyo tunakupa nafasi ya kujieleza na kuomba kura na baadaye ikiwapendeza Waheshimiwa Wabunge wanaweza wakakuuliza maswali yasiyozidi matatu, karibu sana.

**NDG. CHRISANT NYAKITITA NDEGE – MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA DP:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninapenda kuwasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Kazi iendelee.

**NDG. CHRISANT NYAKITITA NDEGE – MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA DP:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii adhimu kusimama mbele yenu na mbele ya Bunge letu Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninapenda kukishukuru chama changu cha *Democratic Party (DP),* kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kusimama mbele ya Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jina langu naitwa Chrisant Ndege Nyakitita, mwanachama wa Chama cha *Democratic (DP),* nina umri wa miaka 52, nimeoa, mke wangu anaitwa Catherine Charles Obudo, nina watoto wanne (wawili wa kiume na wawili wa kike). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu yangu ni elimu ya chuo, pia nina uzoefu katika masuala ya uongozi wa kisiasa kwa maana kwamba nimewahi kuwa Mwenyekiti wa Wilaya wa Chama, Katibu wa Mkoa, Mwenyekiti wa Mkoa katika Chama cha *Democratic* Mkoa wa Mara. Kwa sasa ni Makamu Mwenyekiti Taifa wa *Democratic Party* Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewahi kugombea Ubunge katika Jimbo la Musoma Mjini mwaka 2010, 2015 na 2020. Vilevile nimewahi kushika nafasi mbalimbali za kijamii, lakini nitataja moja ambayo ni Mwenyekiti wa Mtandao wa Marafiki wa Elimu Tanzania, Kanda ya Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, nia yangu kubwa ya kusimama mbele ya Bunge letu Tukufu, kwanza ni kuhakikisha kwamba ninaongoza Bunge nikishirikiana na ninyi kwa maana ya kulisimamia Bunge ili liweze kuielekeza Serikali vizuri kwa maana ya kuishauri, kupitisha bajeti mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyotambua dola yetu ina mihimili mitatu ambayo ni Bunge, Serikali na Mahakama, sasa ili mambo yaweze kwenda vizuri, kazi ya Bunge ni kutunga sheria ambazo ni muhimu na nzuri zenye kufuata maadili ya nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sheria nyingine ni kinzani ambazo wengine wanatulazimisha ili tukizifuata, basi tutapata ile misaada yao. Hata hivyo, mimi nikiwa kama Spika kwa kushirikiana na ninyi Wabunge, tutahakikisha kwamba sheria zote zinazokuja katika Bunge hili ni sheria ambazo zinaendana na maadili ya Mtanzania bila kujali misaada hiyo wanayoweza kutupatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nikiwa kama Spika nitahakikisha na kuona kwamba Bunge hili ninaligeuza kuwa Bunge la maendeleo kwa maana ya kufanya kazi na kazi hiyo inatokana na bajeti zitakazoletwa na Serikali ambapo malengo yake na kama tunavyoelewa, Serikali yetu ya sasa ina mikakati mikubwa ya kuwaletea wananchi maendeleo.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Muda wako unaisha.

**NDG. CHRISANT NYAKITITA NDEGE – MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA DP:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yote nitahakikisha kwamba Bunge linaendelea kuwa tulivu, linafuata maadili na kuifanya nchi yetu kuwa nchi ya amani, upendo na mshikamano.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba kura zenu.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa maelezo yako Ndugu Chrisant Nyakitita Ndege.

Waheshimiwa Wabunge, kama mmemsikia lakini mnayo fursa ya kuuliza kama kuna mtu anataka kuuliza. Mheshimiwa Ester.

**MHE. ESTER A. BULAYA – MBUNGE MTEULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kumuuliza swali mgombea.

Mheshimiwa Mgombea Uspika, moja ya kitu ambacho kinatuongoza katika shughuli za Bunge ambapo Mungu akisaidia tukikuchagua, utatumia Kanuni za Bunge. Je, unaweza ukanitajia Kanuni ya 11(1) na (2) vinasemaje?

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Mimi nadhani kukariri hizo Kanuni ni ngumu sana. Hata sisi wenyewe ukiambiwa utaje Kanuni ya 80 inasema nini ni ngumu. Kwa hiyo, kuna swali lingine? Hakuna, Ndugu Chrisant Nyakitita Ndege, tunakushukuru sana kwa maelezo yako.

**NDG. CHRISANT NYAKITITA NDEGE – MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA DP:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge, ninaomba kura zenu.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Ahsante.

Tunamwomba sasa aingie Ndugu Ndonge Said Ndonge kutoka Chama cha *AAFP (Alliance for African Farmers Party).*

*(Hapa Ndugu Ndonge Said Ndonge – Mgombea kutoka Chama cha Alliance for African Farmers Party (AAFP)aliingia Ukumbuni)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Ndugu Ndonge Said Ndonge, karibu kwenye *microphone* hapo, mkaribishe kwenye *microphone* hiyo, hebu mshushie kidogo maana imekaa juu mno.

Ndugu Ndonge Said Ndonge, karibu sana ndani ya ukumbi wa Bunge na mbele yako humu ndani kuna Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo tunakupa nafasi ya kujieleza kwa dakika zisizozidi tatu na endapo ikiwapendeza Waheshimiwa Wabunge wanaweza wakakuuliza maswali yasiyozidi matatu. Karibu sana ujieleze.

**NDG. NDONGE SAID NDONGE – MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA AAFP:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, leo jina langu umelipatia na sina haja ya kulirudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, nitakuwa Mbunge baada ya kuapishwa hapa. Leo nimesimama hapa kwa lengo moja la kuja kuwa kiongozi katika mhimili huu. *(Makofi/kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya na leo kufikia hapa tulipofikia. Vilevile nitoe pongezi za dhati kwa wananchi wote wa Tanzania kwa kufanya maamuzi yaliyosahihi siku ya Oktoba 29, ambayo imewawezesha wengi wenu kuwepo humu ndani na sisi wengine kuwepo huko nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze tena Mheshimiwa Rais kwa kushinda kwa kishindo kwa asilimia 97. Nawakumbusha mliambiwa msishangilie. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu leo hapa tunaomba ridhaa ya Uspika…

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Jamani naomba tumsikilize.

**NDG. NDONGE SAID NDONGE – MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA AAFP:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake tunaomba ridhaa ya Uspika ili tuwe miongoni mwa viongozi katika Bunge hili, mimi nitajikita katika neno kiongozi. Nitatafsiri neno kiongozi na huo ndiyo utakuwa mwelekeo wangu na nitakuwa natoa mifano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, neno Kiongozi lina herufi zake nane na linaanza na herufi "K". Ile "K" ina maana ya kwamba kiongozi unatakiwa kukosolewa na unaowaongoza. Hili tuna ushahidi kwamba hata Serikali ya Awamu Sita ilipoingia madarakani na ilipokuja ile *DP World,* Mheshimiwa Rais alikubali kukosolewa na aliokuwa anawaongoza, lakini kwa bahati mbaya waliokuwa anawaongoza wenyewe hawakuja na mti dawa, walikuwa wanakosoa tu na hawasemi nini kifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, herufi ya pili ni herufi "I" ina maana ya kuwa ijue tabia ya watu unaowaongoza. Wote hapa ni mashahidi, Mheshimiwa Rais kwa alivyokuwa anajua tabia zetu sisi anaotuongoza, siku ile ya tarehe 3 Novemba baada ya kuapishwa na kutoa ile *lockdown*, watu wote walishangilia na maisha yameendelea. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, herufi ya tatu ni herufi "O"; herufi "O" ina maana ya kwamba onesha kwa vitendo. Kiongozi unapotaka kufanya jambo, basi wewe uwe mstari wa kwanza kuonesha kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, wote sisi ni mashahidi, Mheshimiwa Rais alipokuja wakati anaongoza Awamu ya Sita tulikuwa na *Covid*, alipotaka watalii waje alikuja na *Royal Tour*. Maana yake sasa alikuwa ameonesha kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, herufi nyingine ni herufi "N"; herufi "N" inasema kiongozi unatakiwa unene kauli thabiti. Sisi wote ni mashahidi, hata watu walipokuwa wanasema kwamba Serikali inakopa, lakini Mheshimiwa Rais alisema ni kweli, lakini ni kwa ajili ya nchi na si kwa ajili ya mtu mwingine. Hongera sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, herufi inayofuata ni "G"; ile "G" ina maana gawa madaraka kwa unaowaongoza. Ninyi ni mashahidi, hili kwa Mheshimiwa Rais siyo shida zake. Alimgawia madaraka Mheshimiwa Paul mpaka akayaacha mwenyewe kule Arusha! Pia ninaamini hata mimi kama kura hazitatosha naweza kugawiwa vilevile. *(Makofi/Kicheko)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, herufi inayofuata ni herufi "O"; herufi "O" hii inasema ondoa uonevu kwa unaowaongoza. Sisi wote ni mashahidi, Mheshimiwa Rais alipoingia baada ya kuona manung'uniko akaleta Tume ya Haki Jinai na sisi wote leo tunasema hapa hakuna kukamatwa na Polisi mpaka uchunguzwe. Manung'uniko yameondoka na mambo yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inafuata ile herufi "Z"; zuia migogoro kwa unaowaongoza. Wakati Serikali ya Awamu ya Sita inakuja, kulikuwa na migogoro mingi sana ya wafugaji na wakulima pamoja na watu wa wanyamapori. Mheshimiwa Rais akaja na ile Kamati ya Mawaziri wa Kisekta, wamefanya kazi vizuri na leo migogoro imekuwa adimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, herufi ya mwisho ni herufi (I). Sasa hapa niwambie Waheshimiwa Wabunge, mnapaswa kutembea kifua mbele, kama mtanipa ridhaa ya kuwa Spika katika Bunge hili, nitainua vipato vyenu kwa sababu inasema inua vipato kwa unaowaongoza. Nitainua vipato wenu Waheshimiwa Wabunge ili mkainue vipato vya hao waliopo kwenye Majimbo yenu, ilimradi muendelee kuja huku milele kwa milele.*(Kicheko)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**NDG. NDONGE SAID NDONGE – MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA AAFP:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo, kama hawatajali, waomba ridhaa wenzangu wanaoongozwa na Mheshimiwa Zungu, wanaweza kutangaza kujiondoa ili kazi iwe rahisi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kama wenzangu watakuwa na mgomo kwa neno nililolisema hapo mwanzo, basi ninaomba Wabunge mnipe kura nyingi ikiwezekana na mimi nishinde kwa 97%, ahsanteni sana. *(Kicheko)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Haya, Waheshimiwa Wabunge kuna maswali? Huyu ndiye Ndonge, mnamfahamu bila shaka. Swali la kwanza?

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Swali la pili?

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Swali la tatu?

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Ndugu Ndonge, tunakushukuru sana.

**MBUNGE FULANI:** Amepita. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Aingie sasa Ndugu Amin Alfred Yango, kutoka Chama cha *ADC (Alliance for Democratic Change)*.

*(Hapa Ndugu Amin Alfred Yango Mgombea kutoka Chama cha Alliance for Democratic Change (ADC) aliingia Ukumbini)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Ndugu Amin Alfred Yango kutoka ADC, karibu sana kwenye ukumbi wa Bunge.

**NDG. AMIN ALFRED YANGO – MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA ADC:** Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani sana.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Mbele yako hawa ni Waheshimiwa Wabunge, tunafahamu kwamba umeomba nafasi ya kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, ninakukaribisha utoe maelezo yako kwa dakika zisizozidi tatu, na endapo itawapendeza Waheshimiwa hawa wanaweza wakauliza maswali yasiyozidi matatu, karibu.

**NDG. AMIN ALFRED YANGO – MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA ADC:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana ingawa dakika tatu ninaona kwangu hazitoshi, lakini nitajaribu ku-*summarize*.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Kiti kitaamua, wewe endelea.

**NDG. AMIN ALFRED YANGO – MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA ADC:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majina ninaitwa Amin Alfred Yango…

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** *Microphone* iko mbali kidogo.

**NDG. AMIN ALFRED YANGO – MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA ADC:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majina ninaitwa Amin Alfred Yango, mgombea wa Kiti cha Uspika kutoka Chama cha *Alliance for Democratic Change (ADC)*. Nafasi yangu ni Mkurugenzi wa Mambo ya Nje ama kwa upande wa taaluma mimi ni *Fish Technologist* kutoka Chuo cha *Nyegezi Fisheries,* Mwanza lakini pia *Kunduchi Fisheries College, Dar es Salaam*. Umri wangu ni miaka 55; ni baba wa mwanamke mmoja na watoto watano, ni mzaliwa wa Mkoa wa Mara Wilaya ya Bunda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nijielekeze sasa katika uzoefu katika masuala ya uongozi. Septemba, 1998

nilikuwa *Production Supervisor* wa *TANPH Limited, Mwanza;* mwaka 1999 Meneja Mazingira wa *TANPH* Mwanza; mwaka 2004 *Purchasing Manager TANPH* Mwanza; mwaka 2006 *Assistant Production Manager Sea Product Tanga*; mwaka 2007 *Project Manager Sustainable Tuna Export Project Sea Product Tanga;* mwaka 2007 *Production Manager Sea Product Kilwa Masoko;* mwaka 2009 *Purchasing Manager Royal African Robusta Tropical Limited, 2019 Export Director Hong Kong Live Robusta Export Company Limited.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu wangu katika masuala ya siasa; kama nilivyosema nimekuwa Katibu wa Vijana wa *CUF* Wilaya ya Nyamagana, Mwanza. Kabla ya kuwa Mkurugenzi wa Mambo ya Nje kupitia *ADC* mwaka jana nilikuwa Naibu Mkurugenzi wa Mambo ya Nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nimeamua kugombea nafasi ya Uspika? Sababu ziko nyingi, lakini kwa muhtasari, kama mtanipa ridhaa ya kuongoza Bunge hili nitahakikisha ninasimamia amani na usalama kwa wanaotaka kuhatarisha amani ya nchi na kusimamia umoja wa kitaifa. Pia kwa kuwa kumekuwa na hitajio kubwa la Katiba Mpya basi nitahakikisha kama mtanipa ridhaa Waheshimiwa Wabunge nihakikishe kwamba jambo hili nitalisimamia ndani ya muda mfupi tuweze kupata Katiba Mpya. Vilevile kuondoa Kanuni za Bunge ambazo ni kandamizi ambazo nina imani kuna Waheshimiwa Wabunge ambao wanakuwa na fikra sahihi kabisa za kusaidia nchi, lakini pengine kwa sababu ya kanuni kandamizi wanakuwa wanashindwa kutoa mawazo yao *positive*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa viongozi wangu wa Chama cha *ADC,* hususani Mheshimiwa Shaban Tutu Haji pamoja na kamati yake tendaji kwa kuniteua kuja kugombea nafasi hii adhimu. Mimi si bora kuliko wanachama wote wa *ADC,* lakini wameweza kuniona mimi ninafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitakuwa mchoyo wa fadhila kama nitamaliza *presentation* yangu bila kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi

kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mama Samia Suluhu Hassan hakika amefanya mengi; huko aliko ninadhani ananisikia. Nichukue fursa hii kumpongeza kweli kweli. Nina mengi ya kupongeza lakini jambo la kwanza ni mabadiliko ya mfumo wa uendeshaji katika bandari yetu ya Dar es Salaam. Hiyo ilikuwa ni kichaka cha wahuni, watu walikuwa wanatumia kwa maslahi yao, lakini baada ya kubadilisha mfumo leo rekodi ziko wazi kutoka *TRA* ni sehemu ambayo tunakusanya mapato mengi sana ambayo yanasaidia nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba mama amefanya mengi ambayo siwezi kuyataja kwa muda huu mfupi; lakini amefanya jambo kubwa sana la kusaidia wanyonge kwa kuunda ila kama ya kuratibu haki na amani. Kwa hiyo nimpongeze mama, nimwombee dua ili Mwenyezi Mungu amjaalie, achape kazi, asirudi nyuma sisi tupo nyuma yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho japo si kwa umuhimu mkubwa sana niwashukuru ndugu Waheshimiwa Wabunge wateule wa Bunge hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kwenu na wananchi, wananchi wameonesha imani kubwa kwenu, na nyinyi onesheni imani kwa wananchi ili muweze kuwaletea maendeleo. Shida ya wananchi ni maendeleo na si lingine. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**NDG. AMIN ALFRED YANGO – MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA ADC:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo sasa nichukue fursa hii kuomba kura zenu. Mimi ni mpinzani ambaye nina damu ya kizalendo. Ukinikata damu yangu haitoki nyekundu inatoka ya uzalendo; kwa hiyo nitakuwa mzalendo kwanza. Bunge nitakaloliongoza ikiwa mtanipa ridhaa ni Bunge jumuishi kwamba ni lazima kwa kila hoja itakayokuja tukae tukubaliane kwamba hili tunaliendesha kwa namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuruni, ninaomba kura zenu, mtiki Amin Alfred Yango. Ahsanteni kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Ahsante sana Ndugu Amin.

Waheshimiwa Wabunge, kama kuna mtu anataka kumuuliza mgombea swali. Mheshimiwa Esther.

**MHE. ESTHER N. MATIKO – MBUNGE MTEULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninashukuru kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumuuliza ndugu mgombea wa Kiti cha Uspika; katika maelezo yake alivyojieleza inaonekana ni mtu ambaye anafuatilia sana Bunge na anazijua Kanuni za Bunge na amekwenda mbali kwa kusema kwamba iwapo tutamchagua kwa kura nyingi na akawa Spika wetu ataondoa Kanuni kandamizi za Bunge. Anaweza akawatajia Wabunge hawa ambao ndio watakaompigia kura, je, ni kanuni ipi mojawapo ambayo anaijua ni kandamizi ambayo tukimpa Uspika ataiondoa?

**NDG. AMIN ALFRED YANGO – MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA ADC:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa swali zuri.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Nimekuruhusu jibu tu, endelea kujibu.

**NDG. AMIN ALFRED YANGO – MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA ADC:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Uspika ni taasisi na kwa kanuni za uongozi unapokuwa umechaguliwa kuwa kiongozi kuna kitu kinaitwa *job description* unapewa. Sasa mimi sijawahi kuwa Mbunge, wala sijawahi kuwa Spika ndiyo kwanza nimesimama leo kugombea. Kwa hiyo, nikishaapishwa leo, wakinipa ridhaa na nikiapishwa moja ya kazi kubwa nitakayoifanya ni kila siku usiku na mchana kusoma kanuni kiasi kwamba zikae hapa. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA – MBUNGE MTEULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Ninatamani kumpigia kura mgombea na amejieleza vizuri. Ameeleza shule yake na ameeleza kazi alizozifanya, nimeona anaongelea samaki hadi mpaka mwisho. Sasa nikimwangalia *appearance* mgombea ana nyota mabegani na nikawa najiuliza, majeshi yana *uniform* tofauti. Sasa nikijaribu kuangalia naona kama *Serjeant-At-Arms* sielewi.

Sasa nikataka kujua Mheshimiwa mgombea hizi nyota ulizovaa mabegani ni moja ya *uniform* za kazi yake aliyowahi kufanya au ni *swagga* ya leo aliyokuja nayo Bungeni? *(Kicheko)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amin hilo si swali, hiyo ni *fashion*.

**NDG. AMIN ALFRED YANGO – MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA ADC:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kumsaidia kumjibu.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Unakata kumjibu?

**NDG. AMIN ALFRED YANGO – MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA ADC:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Alaa, haya endelea.

**NDG. AMIN ALFRED YANGO – MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA ADC:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa sina kumbukumbu nzuri ilikuwa tarehe ngapi, *but I still remember,* wakati tunaelekea Uchaguzi Mkuu tuliitishwa kwa Mheshimiwa Msajili wa Vyama tukapewa semina. Moja ya semina tuliyopewa ni ya *Protocol and Leadership* akawa bwana mmoja, *somebody* anaitwa Omary akasema kiongozi ni lazima awe *smart*. Kwa hiyo, rangi isikuhadae Mheshimiwa Musukuma

jirani yangu. Tamu ya chai ni sukari. Haya ni mapambo tu na *smartness. (Makofi)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Haya ninadhani maswali yamekwisha. Tunakuruhusu, na tunakushukuru sana Ndugu Amin; maswali yamekwisha

**NDG. AMIN ALFRED YANGO – MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA ADC:** Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani sana.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Sasa aletwe Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu kutoka Chama Cha Mapinduzi, jaza ujazwe. *(Makofi)*

*(Hapa Mhe. Mussa Azzan Zungu - Mgombea kutoka Chama Cha Mapinduzi aliingia Ukumbini)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Jimbo la Ilala, mbele yako hapa ni Waheshimiwa Wabunge. Tunafahamu umegombea nafasi ya kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano kutoka Chama Cha Mapinduzi. Unapewa dakika zisizozidi tatu za kutoa maelezo na endapo itawapendeza Waheshimiwa Wabunge wanaweza kukuuliza maswali yasiyozidi matatu, karibu sana. *(Makofi)*

**MHE. MUSSA AZZAN ZUNGU – MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA CCM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele yenu ninyi kwenye Bunge hili Tukufu. Mimi ninaitwa Mussa Azzan Zungu nimetia nia ya kugombea nafasi ya Uspika kwenye Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nikishukuru chama changu, Chama Cha Mapinduzi chini ya Mwenyekiti Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kulipendekeza jina langu kwenda kwenye *caucus* ya chama. Niwashukuru wajumbe wa Chama Cha

Mapinduzi kwenye *caucus* kwa kuniteua mimi kuja kuwakilisha katika Bunge hili kama Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya ajenda zangu kuu ni kuliunganisha Bunge hili na wananchi na watu kwa maslahi mapana ya watu, tukishirikiana na Serikali na mhimili wa Mahakama ili tuwe na Taifa moja, Taifa la amani, Taifa ambalo linataka maendeleo na ustawi wao. Serikali chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa unyenyekevu mkubwa wametoa Dira ya Taifa ya 2025-2050. Dira hii itatakiwa isimamiwe vizuri na Bunge hili ili kuisaidia Serikali kutimiza malengo yake ya ustawi wa jamii kwenye afya miundombinu, elimu, amani na ulinzi wa Taifa letu uweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima mkinipa kura zenu nitashirikiana na ninyi kuhakikisha Dira hii ya Taifa iwe na mafanikio makubwa sana ili wananchi wetu waweze kupata hamu, uhuru na starehe na Taifa lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima ninaomba kura zenu. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Katika hatua hii tulisema makofi yapungue kidogo. Haya, ndugu zangu Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu amemaliza kujieleza, kama kuna maswali. Mheshimiwa Ado.

**MHE. ADO SHAIBU ADO – MBUNGE MTEULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu mgombea Mheshimiwa Zungu ningependa kufahamu katika Bunge atakaloliongoza iwapo atachaguliwa kuwa Spika litakuwa na mchango gani katika kuboresha demokrasia nchini Tanzania, hasa katika muktadha wa kujenga muafaka wa kitaifa na kuhakikisha kwamba Tanzania inapata katiba mpya?

**MHE. MUSSA AZZAN ZUNGU – MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA CCM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa swali la Mheshimiwa Ado. Bunge hili litasimamia haki za watu, Bunge hili kama Serikali ilivyotangaza

mchakato wa Katiba Mpya uko njiani na Bunge hili ndilo litakalosimamia Katiba hiyo; na wale ambao watakuwa humu ndani ndio tutakaoamua mustakabali mkubwa wa Taifa letu kwa amani, utulivu na maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Haya swali la pili, swali la tatu, karibu.

**MHE. KANGI A. LUGOLA – MBUNGE MTEULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lilo hapa swali la tatu.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Ahaa, karibu.

**MHE. KANGI A. LUGOLA – MBUNGE MTEULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana.

Mheshimiwa mgombea, siku za nyuma aliwahi kuanzisha sera hapa Bungeni ya jaza ujazwe, sasa nilikuwa ninataka nimuulize, katika Bunge hili la 13 sera hiyo ya jaza ujazwe anaioanisha vipi na Dira ya Maendeleo ya Taifa ambayo ametuambia kwamba ataisimamia kikamilifu?

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zungu hilo swali haliko kwenye Ilani, haliko kwenye Dira lakini kama unapenda kujibu unaweza kujibu.

**MHE. MUSSA AZZAN ZUNGU – MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA CCM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Spika ndani ya Bunge hili yameanishwa kwenye Kanuni ya tolea jipya la mwaka 2025 Kanuni ya nne. Haya ndiyo yatakayokuwa miongozo yangu kwenye Bunge hili. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zungu maswali yameisha sasa…

**MHE. SIGRADA MLIGO – MBUNGE MTEULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti,....

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Ehee, bado una swali? Ulinyoosha ennhe? Haya.

**MHE. SIGRADA MLIGO – MBUNGE MTEULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi.

Napenda kuuliza swali moja; tukimchagua leo akawa Spika wetu wa Bunge, je, ana mkakati gani wa kuhakikisha Bunge hili linakuwa ni Bunge la kuwakilisha wananchi dhidi ya Serikali na si Bunge la kuitetea Serikali? Ahsante.

**MHE. MUSSA AZZAN ZUNGU – MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA CCM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge siyo vita kati ya Serikali na Bunge, pamoja na kuwa Spika anatakiwa kuwa *neutral* lakini niwaase na niwasaidie Waheshimiwa Wabunge, kazi yetu si kuleta kero, shida za wananchi kwenye Taifa letu. Hakuna ugomvi wa Bunge na Serikali wala Bunge na Mahakama. Lengo letu kubwa ni kufanya kazi kwa maslahi ya wananchi si maslahi yetu sisi. Tuwatazame wananchi wetu kwanza na wananchi wetu tutawatazama kwa dira hii mpya iliyotungwa na ambayo ilitolewa na Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan ambayo ni jumuishi. Kwa dira hii tutawafikia wananchi wetu. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa kwa sababu wewe ni Mbunge wa Ilala unaruhusiwa kukaa humu ndani kwa sababu utapiga kura. Ahsante sana. *(Makofi)*

Ndugu zangu tunaingia kwenye hatua ya upigaji wa kura, lakini kabla ya hapo ninamwomba Katibu wa Bunge atuambie tuko wangapi. Ninaomba afanye hesabu kidogo na wale waliopo nje. Mlinzi wetu huku gonga kengele, kuna watu wako nje kidogo, tunataka tuwahesabu, waingie ndani. *Sargeant-At-Arms* angegonga kengele pale wangeingia ndani kidogo. Haya Katibu tuambie, wanaendelea kuhesabu? Sawa.

*(Hapa Wahudumu wa Bunge walihesabu idadi za Wabunge)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Haya humu ndani leo tupo 383, kwa hiyo zoezi la kupiga kura litaanza. Tutagaiwa karatasi ya kupiga kura, karatasi inafanana na hii niliyoishika mimi, ina wagombea sita na kila mgombea kati ya hawa mliowaona ana picha yake kwenye karatasi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, unachotakiwa wewe mpiga kura ni kuweka vema kwenye boksi la mgombea mmoja tu unayempenda wewe. Ukipiga zaidi ya mmoja imechafuka na kura yako ikae ndani ya boksi, ikivuka nje ya boksi imeharibika. Kwa hiyo, Katibu gawa karatasi.

Waheshimiwa Wabunge, jamani ambaye hajapata karatasi anyooshe mkono. Mnaona hiyo mikono eeh? Chima, mnaona mikono ile? Jamani karatasi zimeisha bado kule mikono. Wengi tu hawajapata.

*Hallo,* huyu ameingia sasa hivi. Huyu mteule mmoja. Yuko mmoja, ameandikwa humu? Waliokuja ni watatu tu? Wote?

Waheshimiwa Wabunge, jamani wote tayari mmepiga kura? Bado karatasi kule. Ninyi wagawa karatasi vipi?

Waheshimiwa Wabunge, tunafurahi hata wale walioteuliwa jana na Mheshimiwa Rais wamewahi kupiga kura leo. Ninawaona humu ndani. *(Makofi)*

Jamani ninaomba ambaye hajapata karatasi anyooshe mkono tena. Wote tumepata karatasi?

Waheshimiwa Wabunge, subirini kwanza, ninaomba muwaite hao wagombea wengine ili waone masanduku yetu kwamba yako wazi hapa. Hebu ninyi vijana shikeni hayo masanduku. Wapeni viti nyuma hapo hawa wagombea. Simameni pale katikati. Haya waletwe wale wagombea wengine ambao siyo wajumbe wakae hapo.

Katika hatua hii tunawakaribisha muingie ndani hapo ili mshuhudie hatua inayoendelea. Wameingia wote? Wakae tu hata kwenye viti vyekundu hivyo.

Waheshimiwa Wabunge, ndugu zangu na Waheshimiwa Wagombea mbele yenu kuna hao vijana wetu wawili wameshika masanduku, hebu yaonesheni. Funua mfuniko inamisha chini tuone kama hamna chochote humo ndani.

Haya masanduku mnayaona hayana chochote. Kwa hiyo, kila kitakachoingia humo ndani ni kura kati ya hizo kura 383 mlizozipiga. Ninadhani na ninyi huko nyuma mmeshuhudia. Haya piteni, mmoja kushoto na mmoja kulia tumbukizeni hizo kura humo ndani.

*(Hapa Wahudumu wa Bunge walipita na masanduku ya kura kukusanya kura)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, jamani wote tayari mmeweka kura? Funika kwanza. Ngoja mimi ninapiga kura vizuri. Jamani wote mmetumbukiza kwenye boksi?

Haya Katibu ninataka uya-*seal* haya maboksi yaende kwenye chumba cha kuhesabiwa, lakini weka *seal* kwanza, yafunge kabisa. Haya yapelekwe kwenye chumba maalum na msubiri hapo kwa sababu ninataka kuwaomba wale wawalete wawakilishi. Pelekeni kwenye chumba maalum cha kuhesabia kura.

Waheshimiwa Wabunge, ninawaita mmoja mmoja kati ya wagombea wote sita na ninataka kuwauliza tu. Ndugu Veronica ningeomba kama una mtu wa kukuwakilisha kwenda kuingia kwenye chumba maalum cha kuhesabu kura au kama unaiamini meza hapa. Ndugu Veronica kama kuna mtu wa kukuhesabia kura anaruhusiwa kuingia.

**MBUNGE MTEULE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anaiamini meza.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Unasema?

**MBUNGE MTEULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anaiamini meza.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Anaiamini meza eeh? Haya. Ndugu Anitha kama unataka hata wewe mwenyewe unaweza kuja.

**NDG. ANITHA KHALFAN MGAYA – MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA NLD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwenda mwenyewe.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Haya njoo sogea hapa. Ndugu Chrisant.

**NDG. CHRISANT NYAKITITI NDEGE - MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA DP:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwenda mwenyewe.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Njoo, njoo, njoo.

**MBUNGE MTEULE FULANI:** Anitha ungeacha nikuwakilishe.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Haya Ndugu Ndonge. Msubiriane hapo tutawapeleka. Njoo huku sogea hapo. Ndugu Ndonge.

**NDG. NDONGE SAID NDONGE - MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA AAFP:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Abdallah Ulega. *(Makofi/Vicheko)*

**MBUNGE MTEULE FULANI:** Ulega unaitwa mbele.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Abdallah Ulega simama hapo ukamwakilishe Bwana Ndoge. Ndugu Amin Alfred *(Makofi/Vicheko)*

**NDG. AMIN ALFRED YANGO - MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA ADC:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa Mbunge wangu wa Jimbo la Mwibara, Mheshimiwa Kangi Lugola (Nati ya Kirumi), akaniwakilishe. Bahati mbaya sijamuona.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Anamtaka nani? Kangi Lugola, haya bwana polisi karibu hapa. Nani huyu ni wa Amin huyu eeh? Ndugu Veronica wewe umesema unaiamini meza au unakuja mwenyewe? Haya njoo.

**NDG. VERONICA C. TYEAH - MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA NRA:** Samahani Mwenyekiti, ninamuomba Mbunge wa Singida Mjini, Mheshimiwa Yagi Kiaratu akanisaidie kuhesabu.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Mbunge wa Singida Mjini yuko wapi? Tafuta mwingine huyu hatumuoni humu ndani. Yupo eeh? Ahaa anakuja eeh? Yuko wapi? Ahaa yule Mheshimiwa. Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu.

**MHE. MUSSA AZZAN ZUNGU - MGOMBEA WA NAFASI YA USPIKA WA BUNGE KUTOKA CHAMA CHA MAPINDUZI (CCM):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakwenda mwenyewe. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Haya basi karibu hapa.

Sasa Katibu hebu waelekeze hawa chumba cha kuhesabu kura washuhudie wenyewe. Muongozane na Katibu wa Bunge hapa. Tafadhali mawakala wote muongozane.

Waheshimiwa Wabunge, tunasubiri kazi ya kuhesabu. Nikitoa fursa kila mtu ajitambulishe hapa itachukua muda mrefu?

Sasa kwa ruhusa ya Mwenyekiti maana tumekaa hapa hatujuani juani. Tuna dakika kama 10 hivi au 15 za kuhesabu. Nitoe fursa kuanzia huku kushoto kiti cha kwanza mtu asimame, mimi ni fulani, ni Mbunge Mteule wa jimbo fulani, inatosha.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majina naitwa Agnesta Lambert Kaiza ni Mbunge wa Jimbo la Segerea, CHAUMMA. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Ehe mwingine anayefuata.

**MHE. SIGRADA W. MLIGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majina naitwa Sigrada Wilhem Mligo ni Mbunge wa Viti Maalum CHAUMMA, Mkoa wa Njombe. *(Makofi)*

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Devotha Minja ni Mbunge Viti Maalum CHAUMMA, nawakilisha Mkoa wa Morogoro. *(Makofi)*

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Ado Shaibu, Mbunge wa Tunduru Kaskazini kupitia Chama cha ACT Wazalendo. *(Makofi)*

**MHE. KIZA H. MAYEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Kiza Mayeye, Mbunge wa Jimbo la Kigoma Kaskazini, ACT Wazalendo - Kigoma Kaskazini. *(Makofi)*

**MHE. BAKARI B. SHINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naitwa Bakari Shingo, Mbunge Mteule wa Jimbo la Ukonga, ACT Wazalendo. *(Makofi)*

**MHE. HENRY C. KABEHO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Henry Charles Kabeho, Mbunge Mteule Jimbo la Igunga kutoka Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Zacharia Paulo Issaay Mbunge Jimbo la Mbulu Manyara kutoka Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. DKT. JOHANNES L. LUKUMAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naitwa Daktari Johannes Lembulung Lukumay, Mbunge Mteule wa Chama Cha Mapinduzi, Jimbo la Arumeru Magharibi, Mkoa wa Arusha. *(Makofi)*

**MHE. PATALI S. PATALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majina naitwa Patali Shida Patali ni Mbunge Mteule Jimbo la Mbeya Vijijini kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Jesca David Kishoa, Mbunge wa Iramba Mashariki Mkalama kupitia Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. JACQUELINE C. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majina naitwa Jacqueline Chrisant Mzindakaya ni Mbunge Mteule wa Viti Maalum kutoka Chama Cha Mapinduzi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge Mteule Viti Maalum, Mkoa wa Arusha. *(Makofi)*

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Taska Restuta Mbogo, Mbunge Mteule Viti Maalum Mkoa wa Katavi, Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. JOHN J. NCHIMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaitwa John John Nchimbi ninawakilisha wananchi Jimbo la Nyasa kutoka Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. RASHID HABIB ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Rashid Habib Ali, Mbunge Mteule kutoka Jimbo la Mtambwe kupitia ACT Wazalendo. *(Makofi)*

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Kunti Yusuph Majala, Mbunge wa Jimbo la Chemba, Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. SAID IBRAHIM MZIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Said Ibrahim Mzimba, Mbunge Mteule Jimbo la Mtambile kupitia ACT Wazalendo. *(Makofi)*

**MHE. MBWILO B. KAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Mbwilo Bazilio Kapunda ni Mbunge Jimbo la Nkasi Kaskazini, kupitia ACT Wazalendo. *(Makofi)*

**MHE. JUMA ABDALLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Juma Abdallah Juma, Mbunge Mteule kupitia ACT Wazalendo Jimbo la Tumbe. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED KHALFAN ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Asalaam Aleykum,* naitwa Mohamed Khalfan Issa, Mbunge Mteule Jimbo la Pandani, Kaskazini Pemba kupitia ACT Wazalendo. *(Makofi)*

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Ahmed Juma Ngwali, Mbunge Mteule wa Jimbo la Ziwani kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. SAID HASSAN ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naitwa Said Hassan Ali, Mbunge Mteule Jimbo la Kijini kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. KHAMIS KASSIM ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jina langu ni Khamis Kassim Ali, Mbunge Mteule wa Jimbo la Wawi - CCM. *(Makofi)*

**MHE. ISACK C. JOSEPH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majina naitwa Isack Joseph, Mbunge Mteule Jimbo la Monduli, Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. ASYA ALI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majina naitwa Asya Ali Khamis ni Mbunge Mteule wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Mjini, Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. ARIF S. PREMJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Arif Suleiman Premji ni Mbunge Mteule wa Jimbo la Mtwara Vijijini kupitia tiketi ya CCM. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED MUSSA UTALY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Mohamed Mussa Utaly, Mbunge Mteule wa Jimbo la Lindi Mjini kupitia Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, majina yangu naitwa Condester Mundi Michael Sichalwe, mimi ni Mbunge wa Jimbo la Momba kutokea Mkoa wa Songwe kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Josephine Joseph Kapoma, Mbunge Mteule Viti Maalum kutoka Mkoa wa Morogoro kupitia Chama Cha Mapinduzi. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ABUBAKARI D. ASSENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Abubakari Assenga, Mbunge Mteule wa Jimbo la Kilombero kupitia Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Morogoro. *(Makofi)*

**MHE. KASSIM HASSAN HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Kassim Hassan Haji, Mbunge Mteule wa Jimbo la Mwanakwerekwe Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja kwa Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jina langu ni Salome Wyclif Makamba, Mbunge kutoka Shinyanga kutoka Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. ABUBAKAR MOHAMMED MUSSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jina naitwa Abubakar Mohammed Mussa, Mbunge Mteule Jimbo la Mtoni, Mkoa wa Magharibi Zanzibar. *(Makofi)*

**MHE. MWANAENZI HASSAN SULUHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Mwanaenzi Hassan Suluhu, Mbunge Mteule Viti Maalum - Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. COSMAS M. BULALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Cosmas Mtesigwa Bulala, Mbunge Mteule Jimbo la Kwimba, Mkoa wa Mwanza kupitia Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jina langu ni Daktari Pius Stephen Chaya, Mbunge Mteule wa Manyoni kutoka Singida - Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. THOMAS M. KITIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jina langu ni Chifu Thomas Mgonto Kitima, Mbunge Mteule wa Jimbo la Ikungi Mashariki kupitia Chama Cha Mapinduzi. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. JOEL A. NANAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Joel Arthur Nanauka, ni Mbunge Mteule kutoka Jimbo la Mtwara Mjini kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. DKT. WILSON M. CHARLES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Daktari Wilson Mahera Charles, Mbunge Mteule kutoka Jimbo la Butiama kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Suma Ikenda Fyandomo, Mbunge Mteule wa Viti Maalum kupitia tiketi ya Chama Cha Mapinduzi. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. PASCHAL I. CHINYELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Paschal Inyasi Chinyele, Mbunge Mteule wa Jimbo la Dodoma Mjini. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA I. NASSOR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Halima Iddi Nassor, Mbunge Mteule Viti Maalum - CCM nikiwakilisha wafanyakazi wa sekta binafsi na Serikali. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM A. IBRAHIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Mariam Abdallah Ibrahim, Mbunge Mteule Viti Maalum natokea Mkoa wa Pwani. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. AMINA G. SAID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Amina Good Said, Mbunge Mteule Viti Maalum kutokea Mkoa wa Dar es Salaam - Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. BARAKA ULIMBOKA MWAMENGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Baraka Ulimboka Mwamengo, Mbunge Mteule Jimbo la Kyela kupitia Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. KAKULU B. KAKULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Kakuru Burchard Kakuru, mwakilishi wa Jimbo la Mbagala Dar es Salaam kupitia Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge wa Jimbo la Chamanzi. *(Makofi)*

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Edward Olelekaita Kisau, Mbunge wa Kiteto - Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. ASHA J. FERUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Asha Juma Feruzi, Mbunge wa Viti Maalum Chama Cha Mapinduzi nikiwakilisha Kundi la Vyuo na Vyuo Vikuu. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL J. HAMBAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Emmanuel John Khambay, Mbunge kupitia Jimbo la Babati Mjini kupitia Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Festo Richard Sanga, ni Mbunge wa Jimbo la Makete Mkoa wa Njombe. *(Makofi)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Ester Amos Bulaya, Mbunge wa Jimbo la Bunda Mjini Mkoa wa Mara kupitia Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. ESTER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Esther Nicholaus Matiko, ni Mbunge wa Jimbo la Tarime Mjini kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Katani Ahmadi Katani, Mbunge wa Jimbo la Tandaimba. *(Makofi)*

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Jimbo la Misenyi, Mkoa wa Kagera, Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. NETO P. KAPALATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Neto Paul Kapalata, Mbunge wa Jimbo la Nzega Vijijini Chama Cha Mapinduzi kule kwa mzee maarufu wa nje ya *box*. *(Makofi)*

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jina langu Kitila Alexander Mkumbo, Mbunge Mteule Jimbo la Ubungo - CCM. *(Makofi)*

**MHE. MECKTRIDIS F. MDAKU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majina naitwa Mecktridis Fratern Mdaku, ni Mbunge Mteule wa Jimbo la Malinyi kupitia Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Mteule wa Viti Maalum kundi la Umoja wa Wazazi wa Chama Cha Mapinduzi Tanzania. *(Makofi)*

**MHE. DKT. CATHERINE C. JOACHIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Daktari Catherine Joachim, ni Mbunge Mteule Viti Maalum nikiwakilisha Wazazi, Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. ADONIS A. BITEGEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Adonis Alfred Bitegeko, Mbunge Mteule wa Jimbo la Muleba Kaskazini kupitia Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majina ninaitwa Asia Halamga, Mbunge Mteule Jimbo la Hanang Mkoa wa Manyara. *(Makofi)*

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majina naitwa Ng'wasi Damas Kamani, Mbunge Viti Maalum Kundi la Vijana Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. SALIM MUSSA OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majina naitwa Salim Mussa Omar, Mbunge wa Jimbo la Gando Zanzibar. *(Makofi)*

**MHE. MARIRTA G. KIVUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majina naitwa Marirta Gido Kivunge, Mbunge Mteule Viti Maalum Mkoa wa Arusha. *(Makofi)*

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naitwa Joshua Nassari, ni Mbunge wa watu wa Meru Jimbo la Arumeru Mashariki, Arusha kupitia Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge Mteule Jimbo la Hai Mkoani Kilimanjaro kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Masache Njelu Kasaka, Mbunge wa Jimbo la Rukwa Wilaya ya Chunya kwa Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ndiye Tarimba Abbas, Mbunge wa Jimbo la Kinondoni, Chama Cha Mapinduzi, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Neema Mgaya, Mbunge Viti Maalum kutoka Mkoa wa Njombe. *(Makofi)*

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Livingstone Lusinde Mbunge wa Jimbo la Mvumi Mkoani Dodoma kwa tiketi ya CCM. *(Makofi)*

**MHE. JESCA Y. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Jesca Mbogo, Mbunge Mteule wa Viti Maalum, Mkoa wa Dodoma. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTINA S. MNDEME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Christina Mndeme, Mbunge Mteule Viti Maalum kutoka Mkoa wa Tabora, CCM. *(Makofi)*

**MHE. TINNAR A. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Tinnar Andrew Chenge, Mbunge Mteule Viti Maalum kutoka Mkoa wa Simiyu CCM. *(Makofi)*

**MHE. ABUBAKAR ALI OMARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jina langu naitwa Abubakar Ali Omari, Mbunge Mteule kutoka Jimbo la Manonga, Igunga Mkoa wa Tabora kupitia Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. DOTTO J. BAHEMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majina naitwa Dotto Jasson Bahemu, Mbunge Mteule wa Jimbo la Ngara kupitia Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. KIJAKAZI Y. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Kijakazi Yunus Mohamed, Mwakilishi wa Wanawake wa Mkoa wa Lindi kupitia Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. JUMA M. KAWAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jina naitwa Juma Mustafa Kawamba, ni Mbunge kutoka Jimbo la Igalula Mkoa wa Tabora. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ENG. FADHILI SANDALI CHILOMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majina naitwa Mhandisi Fadhili Sandali Chilombe, ni Mbunge kutoka Jimbo la Tunduru Kusini kupitia Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Elibariki Immanuel Kingu, Mbunge Mteule Ikungi Magharibi. *(Makofi)*

**MHE. AMINA M. MKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaitwa Amina Mussa Mkumba, Mbunge Mteule wa Jimbo la Kibiti kupitia Chama Cha Mapinduzi natoka Mkoa wa Pwani. *(Makofi)*

**MHE. NEEMA P. MAJULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jina naitwa Neema Peter Majule, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Dodoma mwakilishi wa wanawake. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. DEVOTHA D. MBURARUGABA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jina naitwa Devotha Daniel Mburarugaba, Mbunge Viti Maalum, Mkoa wa Kagera kutoka CCM. *(Makofi)*

**MHE. JOHN S. LUHENDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa John Stephano Luhende, Mbunge wa Jimbo la Bukene kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. MHA. MSHAM ALI MUNDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa *Engineer* Msham Ali Munde, Mbunge Jimbo la Liwale kupitia CCM Mkoa wa Lindi. *(Makofi)*

**MHE. ASYA SHARIF OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Asya Sharif Omar, Mbunge Mteule Viti Maalum Chama Cha Mapinduzi natoka Mkoa wa Kaskazini Pemba. *(Makofi)*

**MHE. MARY D. J. SIRATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Mary Daniel Joseph Sirati, Mbunge Mteule Jimbo la Serengeti kutokea Mkoa wa Mara. *(Makofi)*

**MHE. ANTHONY A. MWANTONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Anthony Albert Mwantona, Mbunge Mteule Jimbo la Rungwe, Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. CHIKU A. ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majina naitwa Chiku Athman Issa, Mbunge Mteule wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Arusha kupitia Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. MHA. AMOS W. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa *Engineer* Amos William Maganga, Mbunge Mteule Jimbo la Sikonge - Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naitwa Zainab Rashid Kawawa, Mbunge Mteule wa Viti Maalum

kutokea Mkoa wa Lindi kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majina naitwa Hussein Nassor Amar, *bulldozer* Jimbo la Nyang'hwale niliyetokana na Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. SHAFFIN S. AHMEDALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Shaffin Ahmedali Sumar, Mbunge Mteule Jimbo la Uyui, Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Hapo mbele hapa walijitambulisha? Ninyi mmejitambulisha? Mmeshajitambulisha eeh? Bado?

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Jimbo la Same Mashariki, Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaitwa Nape, Mbunge wa Mtama. *(Makofi)*

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Yahya Mhata, Mbunge wa Nanyumbu. *(Makofi)*

**MHE. PATRICK A. MWALUNENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Patrick Mwalunenge, ni Mbunge Mteule wa Jimbo la Mbeya Mjini kupitia CCM. *(Makofi)*

**MHE. DKT. NGWARU J. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza shikamoo. Mimi ninaitwa Dkt. Ngwaru Jumanne Maghembe, Mbunge wa Jimbo la Mwanga CCM. *(Makofi)*

**MHE. SALEHE M. MHANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Salehe Mbwana Mhando, Mbunge Mteule wa Jimbo la Kilindi, Mkoa wa Tanga kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. ZUBERI Y. MFAUME**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jina ninaitwa Zuberi Yahya Mfaume, ninatokea katika Jimbo la

Morogoro Kusini kule inakopita Barabara ya Bigwa - Kisaki, kupitia Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Ninakumbushwa na Mwenyekiti wetu wa UWT anasema Wabunge wa Viti Maalum mnaotoka kwenye mikondo ya jumuiya, hayo ni mambo yetu, lakini humu ndani semeni Wabunge wa Viti Maalum, Chama Cha Mapinduzi, Wazazi, Vijana haya tuendelee.

**MHE. PROF. RIZIKI S. SHEMDOE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Profesa Riziki Shemdoe, Mbunge wa Jimbo la Lushoto, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JACQUELINE K. ANDREW:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majina ninaitwa Jacquline Kainja Andrew, Mbunge Mteule, Viti Maalum, Mkoa wa Tabora kwa Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Latifa Khamis Juwakali, ni Mbunge Mteule wa Viti Maalum. *(Makofi)*

**MHE. ONESMO M. MNKONDYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majina ninaitwa Mwalimu Onesmo Merdson Mnkondya, Mbunge wa Jimbo la Mbozi, ahsante sana.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Bahati Keneth Ndingo, Mbunge Mteule Jimbo la Mbarali kutoka Mkoa wa Mbeya. *(Makofi)*

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge Mteule kutoka Jimbo la Vwawa, Mkoa wa Songwe. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI DKT. BASHIRU A. KAKURWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Bashiru Ally, Mbunge Mteule wa Kuteuliwa na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi ninaitwa Omar Issa Kombo, Mbunge Mteule wa Jimbo la Wingwi,

Wilaya ya Micheweni, Kaskazini Pemba kupitia Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Emmanuel Peter Cherehani ni Mbunge Mteule wa Jimbo la Ushetu. *(Makofi)*

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Edwin Enosy Swalle, Mbunge wa Jimbo la Lupembe, Mkoani Njombe kwa Chama Cha Mapinduzi.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Issa Ally Mchungahela, Mbunge wa Jimbo la Lulindi kwa Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. SHADYA HAJI OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Shadya Haji Omar, Mbunge Mteule Viti Maalum, Mkoa wa Kaskazini Unguja. *(Makofi)*

**MHE. NABIL AHMED ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Nabil Abdallah, Mbunge wa Jimbo la Dimani, Mjini Magharibi, Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jina langu Haji Amour Haji, Mteule wa Chama Cha Mapinduzi, Jimbo la Pangawe, Zanzibar. *(Makofi)*

**MHE. CORNEL L. MAGEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaitwa Mwalimu Cornel Lucas Magembe, Mbunge Mteule, Jimbo la Chato Kaskazini, Mkoa wa Geita. *(Makofi)*

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Christina Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Shinyanga.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge Mteule, Jimbo la Muleba Kusini – CCM. *(Makofi)*

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge Mteule wa Jimbo la Tabora Mjini kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. ASHA OMAR RASHID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jina langu ni Asha Omar Rashid, Mbunge Mteule wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Mkoa wa Kaskazini Pemba. *(Makofi)*

**MHE. SALUM KHAMIS SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jina langu ni Salum Khamis Salim, Mbunge Mteule Jimbo la Bububu kutoka Zanzibar. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM ANZURUNI MUNGULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Mariam Anzuruni Mungula ni Mbunge Mteule wa Viti Maalum, Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. DKT. SWITBERT Z. MKAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jina langu Switbert Zacharia Mkama, Mbunge Mteule Jimbo la Ukerewe. *(Makofi)*

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Aziza Sleyum Ally, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

**MHE. ASHA R. BARAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Asha Baraka, Mbunge Mteule, Viti Maalum – CCM. *(Makofi)*

**MHE. DKT. ZEYANA ABDALLAH HAMID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Dkt. Zeyana Hamid, Mbunge Mteule, Viti Maalum Zanzibar. *(Makofi)*

**MHE. AMINA ALI MZEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Amina Ali Mzee, Mbunge Mteule – CCM. *(Makofi)*

**MHE. MUSA G. MBUGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Musa Godfrey Mbuga, Mbunge Mteule wa Jimbo la Kisesa, Wilaya ya Meatu, Mkoa wa Simiyu kupitia CCM. *(Makofi)*

**MHE. SILVERY L. SALVATORY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majina ninaitwa Silvery Luboja Salvatory, Mbunge Mteule wa Jimbo la Misungwi, Mkoa wa Mwanza kwa tiketi ya CCM. *(Makofi)*

**MHE. SALIM A. HASHAM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Salim Alaudin Hasham, Mbunge wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Jimbo la Ulanga, Mkoa wa Morogoro. *(Makofi)*

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, majina yangu ni Azza Hillal Hamad, Mbunge wa Jimbo la Itwangi. *(Makofi)*

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Sikudhani Yassini Chikambo, ni Mbunge wa Viti Maalum CCM lakini ni mkazi wa Jimbo la Tunduru Kaskazini lenye kata 24. *(Makofi)*

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jina ninaitwa Tauhida Gallos Nyimbo ni Mbunge Mteule kutoka Mkoa wa Magharibi, Zanzibar. *(Makofi)*

**MHE. ALI KHALIL MIRZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jina ninaitwa Ali Mirza, Mbunge Mteule Jimbo la Kiembe Samaki – CCM. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Jimbo la Ludewa – CCM. *(Makofi)*

**MHE. HAIDERALI H. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Haiderali Hussein Gulamali kutoka Jimbo jipya la Ilongero, Wana-Singida wananiita Basima, Wana-Dodoma wananita Shindishindo, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. CLAYTON R. CHIPANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Clayton Revocatus Chipando, Kigoma wananiita kibarabara, ni Mbunge kutoka Jimbo la Kigoma Mjini niliyeangusha mbuyu. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MHA. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Mhandisi Mwanaisha Ulenge, Mbunge Mwakilishi wa Wanawake wa Mkoa wa Tanga. *(Makofi)*

**MHE. PROF. PIUS Z. YANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, majina yangu ni Profesa Pius Zebhe Yanda, Mbunge Mteule wa Jimbo la Buhigwe, Mkoa wa Kigoma kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. NAOMY D. MWAIPOPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, kwa majina ninaitwa Naomy Duncan Mwaipopo, Mbunge Mteule Viti Maalum kutokea Mkoa wa Kigoma kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Timotheo Mnzava, Mbunge Mteule wa Jimbo la Korogwe Vijijini, Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. ZENA M. KATAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Zena Maulidi Katambo, Mbunge Mteule, Viti Maalum, Mkoa wa Lindi. *(Makofi)*

**MHE. JANETH P. PINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Janeth Peter Pinda, ni Mbunge Mteule wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Katavi kupitia Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Florence George Samizi, ni Mbunge wa Jimbo la Muhambwe kupitia Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. NANCY H. NYALUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Nancy Hassan Nyalusi, Mbunge Mteule wa Viti Maalum, Mkoa wa Iringa. *(Makofi)*

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Kwagilwa Reuben, Mbunge Mteule Handeni Mjini – Tanga.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi, Mkoa wa Simiyu kutoka Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. IMAMU MTUMWA VUAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Imamu Mtumwa Vuai, Mbunge Mteule Jimbo la Magomeni - Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. AMJAD USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Amjad Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni Zanzibar. *(Makofi)*

**MHE. SALUM KHAMIS HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Salum Khamis Haji, Mbunge wa Tunguu, Zanzibar. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED ABDULLA LAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Mohamed Abdulla Laki, Mbunge wa Jimbo la Kwahani, Mkoa wa Mjini Zanzibar. *(Makofi)*

**MHE. SULEIMAN MOHAMED RASHID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Suleiman Mohamed Rashid, Mbunge Jimbo la Mwera kupitia Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. OTHMAN MAULID SULEIMAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jina langu ni Othman Maulid Suleiman, Mbunge Mteule wa Jimbo la Mahonda kupitia tiketi ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. MWINYI JAMAL RAMADHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Mwinyi Jamal Ramadhan, Mbunge Mteule Jimbo la Bumbwini, Zanzibar – CCM. *(Makofi)*

**MHE. KINJEKITILE N. MWIRU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majina ninaitwa Kinjekitile Ngombale Mwiru, Mbunge Mteule Jimbo la Kilwa Kaskazini. *(Makofi)*

**MHE. DKT. REGINA C. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Dkt. Regina Christopher Malima ni Mbunge Mteule

Chama Cha Mapinduzi, ninatokea Mkoa wa Mwanza, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. KHAMIS ALI VUAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Khamis Ali Vuai, Mbunge Mteule Jimbo la Mkwajuni kupitia CCM. *(Makofi)*

**MHE. DKT. RHIMO S. NYANSAHO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Rhimo Semion Nyansaho, Mbunge Mteule wa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

**MHE. MASANJA K. KADOGOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jina ninaitwa Masanja Kungu Kadogosa, Mbunge Mteule kutoka Bariadi Vijijini – CCM. *(Makofi)*

**MHE. WANU HAFIDH AMEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Wanu Hafidh Ameir, Mbunge Jimbo la Makunduchi. *(Makofi)*

**MHE. AMINA IDDI MABROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majina ninaitwa Amina Iddi Mabrouk ni Mbunge Mteule Viti Maalum Mkoa wa Magharibi – CCM. *(Makofi)*

**MHE. NURU I. KASHAKARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majina ninaitwa Nuru Issa Kashakari almaarufu kandahari ni Mbunge Mteule Jimbo la Kigoma Kusini – CCM. *(Makofi)*

**MHE. NASSOR SAID NASSOR MAROO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaitwa Nassor Said Nassor, Mbunge Mteule kutoka Jimbo la Chakechake kupitia Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. HIJA HASSAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Hija Hassan Hija, Mbunge Mteule – CCM Jimbo la Kiwani, Kusini Pemba. *(Makofi)*

**MHE. KHAMIS YUSSUPH HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Khamis Yussuph Hamad, Mbunge Mteule Jimbo la Chonga kutoka Mkoa wa Kusini Pemba – CCM. *(Makofi)*

**MHE. SELINA H. KINGALAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Selina Kingalame, Mbunge Mteule wa Viti Maalum kutoka Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Regina Ndege Qwaray ni Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Manyara, Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Esther Edwin Malleko, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Neema Gerald Mwandabila, Mbunge wa Viti Maalum kutokea Mkoa wa Songwe – CCM, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Chifu Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Tarime Vijijini, Kanda Maalum, kwa kazi maalum, Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. HAIDARY H. SUMRY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote niwashukuru wananchi wa Jimbo la Mpanda Mjini. Kwa majina ninaitwa Haidary Hemed Sumry, Mbunge Mteule wa Jimbo la Mpanda Mjini. *(Makofi)*

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jina ninaitwa Hamoud Abuu Jumaa, Mbunge Mteule wa Jimbo la Kibaha Vijijini, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwa jina ninaitwa Tabasam Hamis Mwagao, Mbunge Mteule Jimbo la Sengerema, tetezi la wanyonge ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Steven Lemomo Kiruswa, Mbunge wa CCM kutoka Jimbo la Longido, Mkoani Arusha. *(Makofi)*

**MHE. DANIEL G. CHONGOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Daniel Godfrey Chongolo, Mbunge Mteule Jimbo la Makambako. *(Makofi)*

**MHE. AISHA M. MDUYAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Aisha Msantu Mduyah, Mbunge Mteule Viti Maalum kupitia Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. RAHMA RIADH KISUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jina langu ninaitwa Rahma Riadh Kisuo, Mbunge Mteule wa Viti Maalum CCM, *thank you. (Makofi)*

**MHE. GEORGE V. LUGOMELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa George Venance Lugomela, Mbunge Mteule Jimbo la Maswa Mashariki – CCM. *(Makofi)*

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jina ninaitwa Hussein Mohamed Bashe, Mbunge Mteule wa Nzega Mjini. *(Makofi)*

**MHE. MAHESH SHAH AKLUSHA BOLISHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Mahesh Shah, Mbunge Mteule, Jimbo la Micheweni, Kaskazini Pemba, Jimbo lenye upendo mkubwa. (Makofi)

**MHE. OMARY M. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Omary Msigwa, Mbunge Mteule wa Jimbo la Madaba kutokea CCM Mkoa wa Ruvuma. *(Makofi)*

**MHE. HASNAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Hasnain Gulamabbas Dewji ni Mbunge wa Kilwa Kusini – CCM.

**MHE. NASSORO RASHID NASSORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Nassoro Rashid Nassoro, Mbunge Mteule wa Jimbo la Konde, Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa tiketi ya CCM. *(Makofi)*

**MHE. MVITA MUSTAFA ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa majina ninaitwa Mvita Mustafa Ali ni Mbunge Mteule

Viti Maalum Mkoa wa Kusini Unguja, mkoa wenye ubora wake. *(Makofi)*

**MHE. MWANTATU MBARAK KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jina ninaitwa Mwantatu Mbarak Khamis, Mbunge Mteule kutoka Mkoa wa Kusini Unguja, Viti Maalum. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Upande huu mmemaliza ehee?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo!

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Haya tuanze hapa, Daktari.

**MHE. DKT. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Selemani Said Jafo, Mbunge Mteule kutoka Wilaya ya Kisarawe, Jimbo la Kisarawe, Mkoani Pwani, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Mohamed Omary Mchengerwa ni Mbunge Mteule wa Jimbo la Rufiji kupitia Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Festo John Dugange, Mbunge Mteule Jimbo la Wanging'ombe kupitia Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. DKT. DOROTHY O. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Dkt. Dorothy Gwajima, Mbunge Mteule kupitia nafasi za Mheshimiwa Rais, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. KABULA E. SHITOBELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Kabula Enock Shitobela, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Mwanza. *(Makofi)*

**MHE. GRACE E. MKOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majina ninaitwa Grace Elias Mkoma, Mbunge Mteule kutoka Mkoa wa Singida – CCM. *(Makofi)*

**MHE. JESCA J. MAGUFULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majina ninaitwa Jesca John Magufuli, Mbunge Mteule wa Viti Maalum kutokea Mkoa wa Geita. *(Makofi)*

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jina ninaitwa Ridhiwani Kikwete Mizega, ninatokea Jimbo la Chalinze – Pwani. *(Makofi)*

**MHE. PASCHAL P. KATAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti na Wabunge Wateule, ninaitwa Patrobass Katambi, Mbunge wa Jimbo la Shinyanga – CCM. *(Makofi)*

**MHE. JACQUELINE K. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge Mteule kupitia tiketi ya Chama Cha Mapinduzi, lakini ninatokea Mkoa wa Ruvuma. *(Makofi)*

**MHE. FADHILI A. LIWAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Fadhili Ally Liwaka, Mbunge Mteule kutoka Jimbo la Nachingwea, Mkoa wa Lindi. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED ABRAHAMAN MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jina langu ni Mohamed Abrahaman Mwinyi, Mbunge Mteule Jimbo la Chambani, Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. PROF. MAKAME MNYAA MBARAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jina langu ninaitwa Makame Mnyaa Mbarawa, Mbunge Mteule kutoka Jimbo la Mkoani, Kusini Pemba, kupitia Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Balozi Dkt. Pindi Chana, Viti Maalum, Njombe. *(Makofi)*

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Innocent Lugha Bashungwa, Mbunge Mteule wa Jimbo la Karagwe kupitia tiketi ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Deus Clement Sangu, Mbunge Mteule kutoka Jimbo la Kwela, Mkoa wa Rukwa, kupitia Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Daniel Baran Sillo, Mbunge Mteule wa Chama Cha Mapinduzi, Jimbo la Babati Vijijini. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa George Natany Malima, Mbunge Mteule Jimbo la Mpwapwa. *(Makofi)*

**MHE. DICKSON N. L. VILLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaitwa Dickson Nathan Lutevele, maarufu kwa jina la Villa. Mimi ni Mbunge Mteule wa Jimbo la Mafinga Mjini, Wilayani Mufindi. *(Makofi)*

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa David Mathayo David, Mbunge Mteule wa Jimbo la Same Magharibi, Mkoa wa Kilimanjaro, Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Mhandisi Godfrey Kasekenya, Mbunge Mteule Jimbo la Ileje, Mkoa wa Songwe. *(Makofi)*

**MHE. DKT. JUMA Z. HOMERA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majina ninaitwa Dkt. Juma Zuberi Homera, Mbunge Mteule wa Jimbo la Namtumbo, Mkoani Ruvuma. Karibuni sana na atakaye aje. *(Makofi)*

**MHE. ALLY HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Ally Hassan King, Mbunge wa Jang'ombe. *(Makofi)*

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Abdallah Dadi Chikota, ni Mbunge Mteule wa Jimbo la Nanyamba - CCM. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge Mteule Jimbo la Peramiho, Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majina ninaitwa Deogratius John Ndejembi, Mbunge Mteule wa Jimbo la Chamwino hapa Mkoani Dodoma. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majina ninaitwa George Boniface Simbachawene, Mbunge Mteule wa Jimbo la Kibakwe, Mkoa wa Dodoma, Wilaya ya Mpwapwa kupitia Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Abdullah Ali Mwinyi, Mbunge Mteule, nafasi 10 za Rais. *(Makofi)*

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Njalu Daudi Silanga, Mbunge Mteule, Jimbo la Itilima. *(Makofi)*

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Eric Shigongo James, Mbunge wa Jimbo la Buchosa, Sengerema Mwanza kupitia Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Alhaji Dkt. Hamisi Shabani Taletale, Mbunge wa Morogoro, Kusini-Mashariki kupitia Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Mwantumu Zodo, Mbunge Mteule Viti Maalum Mkoa wa Tanga. *(Makofi)*

**MHE. DKT. TULIA ACKSON:** Ahsanteni sana. Ninaitwa Tulia Ackson, Mbunge wa Jimbo jipya la Uyole. *(Makofi)*

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majina ninaitwa James Kinyasi Millya. Mpaka leo ni Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki, pia ni Mteule wa Jimbo la Simanjiro kupitia CCM. *(Makofi)*

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Zainab Katimba, Mbunge wa Viti Maalum kupitia Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. DOUGRAS O. D. MASSABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Ojambi Didas Massaburi, Mteule Jimbo jipya la Kivule, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Mariam Ditopile Mzuzuri, Mbunge wa Jimbo la Kondoa Mjini. Nimebahatika kuwa Bungeni hapa kipindi cha tatu kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, lakini ndio kipindi cha kwanza nimegundua kumbe Ubunge una cheti. Kwa hiyo, hongereni sana wenye vyeti. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Deo Mwanyika, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini, CCM. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Martha Festo Mariki, Mbunge Mteule kutoka Mkoa wa Katavi, Viti Maalum. *(Makofi)*

**MHE. LUTENGANO G. MWALWIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Lutengano George Mwalwiba, Mbunge Mteule wa Jimbo la Busokelo, Mkoa wa Mbeya, Wilaya ya Rungwe kutokea CCM. *(Makofi)*

**MHE. DAVID M. KIHENZILE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge Jimbo la Mufindi Kusini kupitia CCM, Mkoani Iringa. *(Makofi)*

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Ritta Kabati, Mbunge wa Jimbo la Kilolo kupitia Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Aysharose Mattembe, Mbunge kutoka Mkoa wa Singida kupitia Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Judith Salvio Kapinga, Mbunge wa Jimbo la Mbinga Vijijini kutokea Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Salma Rashid Kikwete, Mbunge Mteule Jimbo la Mchinga. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ABDUL YUSSUF MAALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Abdul Yussuf Maalim, Mbunge Mteule wa Jimbo la Amani Zanzibar kupitia CCM. *(Makofi)*

**MHE. MUHSIN HAJI USSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Muhsin Haji Ussi, Mbunge Mteule wa Jimbo la Malindi, Zanzibar kupitia tiketi ya Chama Cha Mapinduzi. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED KASSIM SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jina ninaitwa Mohamed Kassim Salum, umaarufu wangu Morgan kutokea Jimbo la Mpendae, Mkoa wa Mjini Unguja, Zanzibar, kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. DKT. JAFAR R. SEIF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majina ninaitwa Dkt. Jafar Rajab Seif, Mbunge kutokea Jimbo la Busanda kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI MAHMOUD THABIT KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Mahmoud Thabit Kombo, Mteule wa Mheshimiwa Rais. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ENG. KUNDO A. MATHEW:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa *Engineer* Kundo Andrea Mathew, Mbunge wa Bariadi Mjini kutoka Mkoa wa Simiyu kupitia Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. JOHN F. NZILANYINGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti pamoja na Wabunge, ninaitwa John Fransisco Nzilanyingi, Mbunge Mteule wa Jimbo la Nyamagana, Mkoa wa Mwanza nikiwakilisha Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. MOSES C. BUJAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, majina yangu ni Moses Bujaga, Mbunge Mteule wa Jimbo la Sumve, Mkoa wa Mwanza, Chama Cha Mapinduzi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Zimeni hizo *microphones.* Tuendelee, tumalizie hapo.

**MHE. KAFITI W. KAFITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majina ninaitwa Kafiti William Kafiti, Mbunge Mteule wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Jimbo la Ilemela, Mwanza. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Huyo anayesimama sasahivi atamtambulisha huyo mama mezani.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR K.n.y. MHE. NASRIA NASRY ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Nasria Nasry Ally, ni Mbunge wa Viti Maalum, Watu Wenye Ulemavu, Zanzibar, kupitia Chama Cha Mapinduzi. Mheshimiwa Nasria ana changamoto ya kutosikia, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ARON N. FAGASON:** Mheshimiwa Mwenyekiti, majina yangu ni Fagason Aron Nkingwa, Mbunge Mteule wa kutoka Mkoa wa Geita, Jimbo la Mbogwe, CCM, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. KIJA L. NTEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majina ninaitwa *Engineer* Kija Limbu Ntemi, Mbunge Mteule wa Jimbo jipya zuri kabisa la Katoro, Mji Mdogo, pale palipokuwa na Kariakoo ambayo haipo Geita ni Katoro peke yake. Karibuni sana Katoro. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Ndugu zangu ningependa tumalize wote, lakini bado wewe?

Ninataka tumalizie zoezi lililotuleta kwanza. Tupate matokeo halafu baadaye, ikimpendeza Mheshimiwa Spika tunaweza tukamalizia upande huu. *(Makofi)*

Haya. Ninaomba Katibu aingie.

**MBUNGE FULANI:** Watajitambulisha saa ya kuapa.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Lakini imefurahisha kidogo, maana najua mngeenda kunywa chai kule.

Haya, Katibu tafadhali, hebu soma matokeo.

**MATOKEO YA KURA**

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Ninaomba kusoma matokeo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya kura zilizopigwa ni 383, idadi ya kura zilizoharibika ni tatu. Wale wagombea wawili, akinamama, kuna Waheshimiwa imewapendeza kupiga kura mbili mbili, wamewapigia wote kwenye karatasi moja.

Idadi ya kura kwa wagombea.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Hawasikii. Hiyo *microphone* yako ukiifunua hivi unasikika vizuri zaidi.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante ninaomba kurudia; idadi ya kura zilizopigwa ni 383, idadi ya kura zilizoharibika ni tatu. Hizi zimetokana na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kuwapigia wagombea wawili kwenye karatasi moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya kura kwa kila mgombea ni kama ifauatavyo; Ndugu Veronica Charles Tyeah wa *NRA* kura sifuri; Ndugu Chrisant Nyakitita wa *DP* kura sifuri; Ndugu Amin Alfred Yango wa *ADC* kura sifuri; Ndugu Anitha Khalfan Mgaya kura moja; idadi ya kura za Ndugu Ndonge Said Ndonge wa *AFP* kura moja; na idadi ya kura kwa Ndugu Mussa Azzan Zungu ni 378. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, hivyo, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu amechaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jumla ya kura 378. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaomba iingie kwenye rekodi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu amechaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jumla ya kura 378. Matokeo haya yamethibitishwa kwa kusaini kwa baadhi ya wagombea na wasimamizi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Ahsante sana Katibu.

Sasa kabla hatujamuita Mheshimiwa Zungu ili aweze kupata kiapo mbele yetu, kwa ruhusa yenu, ningependa niwaite wale wagombea wengine niwape angalau dakika moja moja, kama ikiwapendeza.

**MBUNGE FULANI:** Mwenyekiti muda.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Angalau mmoja kwa niaba yao.

**MBUNGE FULANI:** Hapana Mwenyekiti muda.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Haya.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mgombea mmoja sawa kwa sababu ya orodha ndefu ya Wabunge kuapa leo. Mmoja sawa.

**MBUNGE FULANI:** Na tungependekeza aje Anitha.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Anitha.

**MBUNGE FULANI:** Said Ndonge.

**MBUNGE FULANI:** Huyo aliyepata kura moja.

**MBUNGE FULANI:** Tumpe Ndonge, aliyepata kura.

**MBUNGE FULANI:** Mwenyekiti, Anitha.

**MBUNGE FULANI:** Ndonge.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumpe Ndonge.

**MBUNGE FULANI:** Mwanamke kwanza.

**MBUNGE FULANI:** Anitha.

**MBUNGE FULANI:** *Ladies first,* Anitha.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Taarifa.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Ndugu Anitha bila shaka unajua hata wenzako wangesema nini. Tukupatie dakika moja angalau useme kidogo kwa niaba ya wagombea wenzako.

**NDG. ANITHA KHALFAN MGAYA – MGOMBEA WA NAFASI YA SPIKA KUTOKA CHAMA CHA NLD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya wagombea wenzangu, mimi Anitha Khalfan Mgaya, tunashukuru sana na tunawapongeza. Muendelee kupigania nchi yetu. Pamoja na yote mum-*support* Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika harakati zake zote za kuhakikisha nchi inakuwa salama, yenye usawa na upendo mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Ahsante sana Ndugu Anitha. Ninadhani tumesema mmoja kwa niaba ya wote.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa *gender.*

**MBUNGE FULANI:** Ndonge.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Basi Waheshimiwa Wabunge.

**MBUNGE FULANI:** Anitha, namba ya simu. *(Kicheko)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunashukuru sana kwa kukamilisha zoezi hili. Wagombea tunawashukuru sana kwa kukamilisha zoezi hili vizuri sana.

Sasa namuita mbele yenu mgombea wa Chama Cha Mapinduzi, Ndugu Mussa Azzan Zungu.

*(Hapa Spika Mteule Mhe. Mussa A. Zungu Aliingia Ukumbini)*

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, ninayo heshima kukuarifu kwamba Wabunge wa Bunge hili Tukufu katika kutekeleza masharti ya Ibara ya 84(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wamekuchagua wewe Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu uwe Spika wa Bunge hili. Kwa hiyo basi, kutokana na kuchaguliwa kwako, sasa nakuita wewe Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu uape viapo vinavyohusika.

Karibu.

## KIAPO CHA UAMINIFU NA TAMKO LA AHADI YA UZALENDO

Mhe. Mussa Azzan Zungu

## KIAPO CHA UAMINIFU, TAMKO LA AHADI YA UZALENDO NA KIAPO CHA SPIKA

**MHE. MUSSA AZZAN ZUNGU:** Mimi, Mussa Azzan Zungu, nathibitisha kwamba nitakuwa mwaminifu kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuitumikia kwa moyo wangu wote na kwamba nitaihifadhi, nitailinda na kuitetea Katiba ya Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa sheria iliyowekwa. Ewe Mwenyezi Mungu nisaidie. *(Makofi)*

Mimi, Mussa Azzan Zungu, kwa heshima kubwa ninaahidi mbele ya Bunge Tukufu kuwa, nitakuwa mtiifu na mwaminifu kwa nchi yangu Tanzania na kwamba ninaahidi kuilinda, kuitumikia na kuitetea Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa nguvu zangu zote na moyo wangu wote. Ewe Mwenyezi Mungu, nisaidie. *(Makofi)*

Mimi, Mussa Azzan Zungu, nathibitisha kwamba nitaitumikia vema na kwa moyo thabiti Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kazi zangu kama Spika wa Bunge, na katika kutimiza wajibu wa cheo hicho nitawatendea haki watu wote kwa mujibu wa Katiba, Kanuni za Bunge, na Sheria, Mila na Desturi za Jamhuri ya Muungano na kwa vyovyote vile sitatoa siri za Bunge. Ewe Mwenyezi Mungu nisaidie. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliima wana imani na Spika Mhe. Mussa Azzan Zungu)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Ndugu zangu, kazi iliyotuleta leo asubuhi imeisha. Kwa kazi tuliyoifanya tumekamilisha *process* yote ya kumchagua Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa matokeo yaliyosomwa na Katibu wa Bunge, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu kutoka Chama Cha Mapinduzi ndiye Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninawashukuru wote waliokuja humu ndani kusikiliza na kuona hii *process* ya kidemokrasia, hapa ndiyo mwisho, tumemaliza shughuli hii. Kwa sasa ninamwomba Mheshimiwa Spika aende akajitayarishe ili aje akae kwenye Kiti chake aendeshe Bunge rasmi. *(Makofi/Vigelegele)*

*(Hapa Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alitoka ndani ya Ukumbi wa Bunge)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI – MWENYEKITI:** Wakati ninawashukuru wageni wote nimesahau kumshukuru mke wangu yupo hapa, Germina Lukuvi pamoja na wageni wengine. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana kwa ushirikiano wenu na cheo changu kimefutwa rasmi. *(Kicheko/Makofi)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. William V. Lukuvi) aliondoka kwenye Kiti*

*Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alirejea Ukumbini*

**WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI**

*(Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki Ziliimbwa)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**TAARIFA YA SPIKA**

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hotuba fupi ya Spika ya shukrani kwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 10(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, tarehe 11 Novemba 2025.

Waheshimiwa Wabunge Wateule, awali ya yote ninaomba kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kutujalia kufika leo tarehe 11 Novemba, 2025 ambayo ndiyo Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Kwanza wa Bunge la 13.

Waheshimiwa Wabunge Wateule, kwa kuwa ndiyo ninasimama kwa mara ya kwanza nikiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa namna ya pekee ninakishukuru chama changu Chama Cha Mapinduzi chini ya uongozi imara wa Mwenyekiti wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniamini na kunipendekeza kuwa mgombea wa nafasi hii ya kuliongoza Bunge. Siyo kwamba mimi ni bora kuliko wenzangu wote waliogombea kupata nafasi hii katika ngazi ya chama, lah hasha! Kwa mapenzi yake Mwenyezi Mungu alinipa kibali na kuridhia nigombee nafasi hii. Ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Aidha, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge Wateule wote kwa kunipigia kura na kuniamini kuwa kiongozi wenu mkuu wa Bunge. Imani mliyoonesha kwangu ni kubwa, ninathamini sana imani hiyo, ninawahakikishia kuwa huu ushindi ni wetu sote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge Wateule, hamjanichagua tu ili niongoze Bunge, bali mmenichagua ili tufanye kazi pamoja, niwatumikie ninyi na kuhakikisha yale yote tuliyokubaliana na tutakayokubaliana kama vipaumbele vya Taifa katika mipango yetu mbalimbali kwa kipindi cha miaka mitano ijayo, yafanikiwe kwa maslahi mapana ya kuwatumikia wananchi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Ninawaahidi kuwa kutakuwa na Bunge moja litakalotoa fursa sawa kwa Waheshimiwa Wabunge wote na kwamba Ofisi ya Spika itakuwa wazi kwa kila Mbunge kwa ushauri mbalimbali. *(Makofi)*

Aidha, ninawashukuru watangulizi wangu katika nafasi hii ya Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hususan Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani ambaye amekuwa kiongozi wangu akiwa Spika na mimi nikiwa Naibu Spika katika Bunge la 12, kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2022 – 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dkt. Tulia aliniamini na kunishirikisha katika masuala mbalimbali na nilitii maelekezo yake yote ili kuhakikisha Bunge letu linatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa kanuni na taratibu zilizopo. Ninakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Tulia kwa mchango wako, mafunzo na elimu uliyonipa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge Wateule, kwa muktadha huo, ninawaahidi viongozi watakaochaguliwa kuwa wasaidizi wangu, Naibu Spika na baadaye Wenyeviti wa Bunge, kwamba tutashirikiana kuliongoza Bunge hili la 13 kwa kutoa maamuzi ya haki kwa kuzingatia uadilifu na kutokuwa na upendeleo wowote, kuongoza kwa Katiba, Sheria za nchi, na Kanuni za Kudumu za Bunge kwa vyama vyote vyenye uwakilishi Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge Wateule, ingawa bado hatuna upande wa Serikali leo, tunae Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Hamza Johari, ninaahidi kutoa ushirikiano kwa Serikali kwamba kama Bunge tutashauri na kutoa Maazimio ya Bunge kwa ajili ya ustawi wa wananchi na maendeleo endelevu ya nchi yetu. *(Makofi)*

Ninamshukuru pia Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard na timu yake yote ya watumishi wa Bunge kwa maandalizi mazuri ambayo yametuwezesha leo kuanza kikao chetu cha kwanza cha Mkutano wa Kwanza wa Bunge la 13. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge Wateule, kipekee sana ninawashukuru wananchi wa Jimbo la Ilala kwa kuniamini na kunichagua kuwa Mbunge wao kwa kipindi cha tano sasa, ninawashukuru sana kwa heshima kubwa mliyonipa. Hakika nina deni kubwa sana kwenu, wema hulipwa kwa wema. *(Makofi)*

Ninaushukuru sana uongozi wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam na Wilaya ya Ilala pamoja na viongozi wengine wote kwa heshima kubwa waliyonipa na ushirikiano wanaoendelea kunionesha. *(Makofi)*

Mwisho lakini si kwa umuhimu, ninaishukuru familia yangu, imesimama na mimi katika nyakati zote. Dua zao, upendo na

uvumilivu wao ndivyo vilivyonibeba na kunifanya kuendelea kuwa imara katika kuwatumikia wananchi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge Wateule, muda mchache ujao mnakwenda kuapa Kiapo cha Uaminifu, ninawapongeza sana kwa kuaminiwa na kuchaguliwa na wananchi ili kuwawakilisha Bungeni. Kwa pamoja tushirikiane ili kulinda imani hiyo kubwa tuliyopewa na wananchi. Ninawashukuru sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**KIAPO CHA UAMINIFU NA TAMKO LA AHADI YA UZALENDO**

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Kiapo cha Uaminifu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* - KATIBU MEZANI*:***

1. Mhe. Dkt. Tulia Ackson
2. Mhe. Dkt. Doto Mashaka Biteko

**MBUNGE MTEULE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge Wateule, tunaomba utulivu ndani ya Bunge.

3. Mhe. William Vangimembe Lukuvi

**MBUNGE FULANI MTEULE:** Kuhusu Utaratibu.

**MBUNGE FULANI MTEULE:** Wewe nyamaza.

4. Mhe. Najma Murtaza Giga
5. Mhe. Deodatus Philip Mwanyika
6. Mhe. Hamza Saidi Johari
7. Mhe. Salma Rashid Kikwete

*(Wabunge Waliotajwa Hapo Juu Waliapa Kiapo cha Uaminifu na Tamko la Ahadi ya Uzalendo)*

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:** Waheshimiwa Wabunge, nitasoma majina kwa makundi kwa kuzingatia orodha iliyopo leo na muda. Wabunge watakaosomwa watakaa kwenye viti vya mbele mkono wa kulia kwa Spika na wataapa kwa mfuatano nitakaokuwa nikiusoma. Naanza na: -

8. Mhe. Juma Abdalla Juma
9. Mhe. Abdallah Dadi Chikota
10. Mhe. Abdallah Hamis Ulega
11. Mhe. Abdallah Jafari Chaurembo
12. Mhe. Abdul Yussuf Maalim

*(Wabunge Waliotajwa Hapo Juu Waliapa Kiapo cha Uaminifu na Tamko la Ahadi ya Uzalendo)*

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:** Waheshimiwa Wabunge, nitasoma majina mengine matano, halafu matano baada ya hayo matano nitayasoma ili waliopo upande huu wasogee upande wa kulia kwa Mheshimiwa Spika. Niaanza na:-

13. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa
14. Mhe. Wanu Hafidh Ameir
15. Mhe. Jenista Joakim Mhagama
16. Mhe. Joseph Kasheku Musukuma
17. Mhe. Dougras Didas Massaburi

*(Wabunge Waliotajwa Hapo Juu Waliapa Kiapo cha Uaminifu na Tamko la Ahadi ya Uzalendo)*

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

18. Mhe. George Boniface Simbachawene
19. Mhe. Abubakar Alli Omar
20. Mhe. Abdul-Aziz Mohamed Abood

21. Mhe. Abubakari Damian Asenga
22. Mhe. Abubakar Mohammed Mussa
23. Mhe. Ado Shaibu Ado
24. Mhe. Prof. Adolf Faustine Mkenda
25. Mhe. Adonis Alfred Bitegeko
26. Mhe. Aeshi Khalfan Hilaly
27. Mhe. Agnes Elias Hokororo

*(Wabunge Waliotajwa Hapo Juu Waliapa Kiapo cha Uaminifu na Tamko la Ahadi ya Uzalendo)*

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:** Waheshimiwa Wabunge, nitakao wasoma ambao wapo mkono wa kushoto mnakumbushwa kutokukatisha mbele ya Siwa. Nawasoma Wabunge kumi; wataanza watano kukaa kwenye viti, watano watajiandaa, lakini wakiwa mkono wa kulia kwa Spika:-

28. Mhe. Agnes Mathew Marwa
29. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza
30. Mhe. Ahmed Ally Salum
31. Mhe. Ahmed Juma Ngwali
32. Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby
33. Mhe. Aisha Msantu Mduyah
34. Mhe. Alan Thomas Mvano
35. Mhe. Salim Alaudin Hasham
36. Mhe. Hussein Mohamed Bashe
37. Mhe. Salum Khamis Salum
38. Mhe. Ali Haidar Madeweyya
39. Mhe. Ali Hassan Omar King
40. Mhe. Ali Khalil Mirza
41. Mhe. Khamis Ali Vuai
42. Mhe. Ally Yahya Mhata
43. Mhe. Kassimu Amari Mbaraka
44. Mhe. Amina Ali Mzee
45. Mhe. Isaya Moses Mngurumi
46. Mhe. Amina Good Said

*(Wabunge Waliotajwa Hapo Juu Waliapa Kiapo cha Uaminifu na Tamko la Ahadi ya Uzalendo)*

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwa orodha ya sasa tumemaliza.

Mheshimiwa Spika, ninasoma majina kumi watakaoanza kuapa mchana; Mheshimiwa Amina Iddi Mabrouk, Mheshimiwa Amina Mussa Mkumba, Mheshimiwa Amjadi Ussi Salum Pondeza, Mheshimiwa *Engineer* Amosy William Maganga, Mheshimiwa Amour Seif Abdalla, Mheshimiwa *Engineer* Andrea Kundo Mathew, Mheshimiwa Angellah Jasmine Mbelwa Kairuki, Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninawashukuru sana, tunaahirisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni ya leo.

*(Saa 7.20 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## TAARIFA YA SPIKA

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza nichukue nafasi hii kuwapongeza sana kwa umakini wenu, kwa hoja zenu, kwa kuwajua kweli mmekomaa kwenye kuapishwa leo asubuhi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna mambo mapya yameanza leo na siyo ninyi, hata wananchi mitaani kwao lilikuwa jambo geni. Bunge letu ni Bunge ambalo linafuata miongozo mbalimbali, lakini nilitaka niseme hivi kwa kuwapongeza kwa *concern* ambayo mliiona; kuna watu walitaka kuomba utaratibu. Sikutaka kuingilia, kwa sababu ningeweza vilevile kuwauliza utaratibu kwa Kanuni ipi? Mngeshindwa kusema kwa hiyo, nikasema niwape heshima yenu, lakini mmenifurahisha sana kwa ukomavu wenu na uwezo wenu kwa kujua kipi kiende au kipi kisiende. Sasa nina maelezo hapa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninatumaini kila mmoja amepatiwa Nakala ya Kanuni za Kudumu za Bunge za 2025 na Kitabu cha Sheria mbalimbali zinazotumika katika uendeshaji wa Shughuli za Bunge 2025. Hizo ni zana muhimu zinazotuongoza katika kutekeleza majukumu ya Bunge hili. Ninatoa wito kwa kila mmoja kuzisoma, kuzielewa na kutekeleza masharti yaliyowekwa na sheria na kanuni hizo.

Waheshimiwa Wabunge, wakati wa kikao cha asubuhi baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hawakuzingatia masharti ya Kanuni ya 76(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge 2025. Kanuni hiyo inaweka masharti kuwa, kila Mbunge ana wajibu wa kutulia na kukaa kwa heshima mahali pake. Aidha, Kanuni hiyo inazuia Mbunge kutoka mahali pake na kupita mbele, pembeni au kuizunguka Siwa. Ifahamike kwamba Siwa inapokuwa imewekwa kwenye meza, mbele ya Kiti cha Spika inaashiria Mamlaka ya Bunge, hivyo ni lazima mamlaka hayo yaheshimiwe.

Waheshimiwa Wabunge, mara baada ya Spika kuapishwa, anakuwa na mamlaka ya kutekeleza majukumu ya Spika ikiwepo kuongoza Vikao vya Bunge akiwa ameketi kwenye kiti chake; ikiwa ni pamoja na kikao cha kuapisha Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, huu ni utaratibu uliozoeleka katika Mabunge ya nchi za Jumuiya ya Madola, wakati wa kuapisha Wabunge Spika anaweza kusimama mbele ya Meza ya Spika au kubaki ameketi katika kiti chake. Asubuhi nilisimama kwa sababu

niliwapa heshima, ndiyo mwanzo mwanzo. Tumeelewana jamani? *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa Kanuni ya 5 ya Kanuni za Kudumu za Bunge 2025 inaeleza kwamba; "Wakati wa kuendesha Shughuli za Bunge, Bunge letu pamoja na mambo mengine, huzingatia mila na desturi za Mabunge mengine." Ule utaratibu wa Kibunge unafanana na utaratibu wa Bunge la Tanzania. Kuna Mabunge wanaapishwa watu kumi kumi, yapo ya madola; kuna Mabunge wanaapishwa Bunge zima, kila mmoja anapewa hati ya kiapo, hamtazami Spika, wanatazamana wenyewe kwa wenyewe. Hizo ndizo Kanuni za Jumuiya ya Madola.

Waheshimiwa Wabunge, kwa maelezo hayo, Bunge letu linaweza kutumia utaratibu wa kuwaapisha Waheshimiwa Wabunge Wateule Spika akiwa ameketi katika kiti chake au akiwa amesimama mbele ya Meza ya Spika kama inavyofanyika katika Mabunge ya nchi za Jumuiya ya Madola, Tanzania ikiwa ni nchi mojawapo. Hivyo, ninawakumbusha kusoma na kuzingatia kanuni zetu.

Spika anapitishwa na Wabunge bila kuapa. Si mmeona leo? Mmenichagua mimi, ninyi hamkuapa, tofauti na Mamlaka ya Serikali. Kwa hiyo, Bunge tusilifananishe na mamlaka kubwa ya nchi ya Serikali; Mheshimiwa Rais akishaapishwa na yeye ndiyo anaapisha Wabunge wengine. *(Makofi)*

Mambo yako mengi, ninataka niyapunguze punguze kwa sababu nyinyi ni wazoefu mtaelewa upesi sana. Vilevile, mara nyingi tunasema, Spika siyo kocha, Spika ni *referee* na mimi kama *referee* kanuni zangu za mpira ziko 17, hizi hapa. Kwa hiyo, ni lazima mwelewe tofauti ya namna gani kiti kinavyofanya kazi na ninyi Wabunge wa zamani mnajua, Wabunge wapya vilevile mnajua. Mnafuatilia sana mambo haya ndiyo maana mmepata sifa ya kuingia ndani ya Bunge hili. Hongereni sana. Kwa hiyo, ninawaomba sana. *(Makofi)*

Leo tumechelewa kwa sababu ya mambo mengi, lakini pamoja na kuchelewa, baadhi ya Wabunge wakiambiwa kuja upande huu wanasita au wanakuja kwa wanavyotaka wao wenyewe, siyo sahihi. Tujaribu kumaliza hili, ilikuwa leo tuwaapishe watu 230; mpaka sasa hivi tumewaapisha watu 50 tu.

Kwa hiyo, ninawaomba sana, Wabunge ambao tayari wanajua orodha yao ya kuapishwa muhamie upande huu ili zoezi tulifanye kwa haraka ili leo na kesho tumalize, Alhamisi twende kwenye ratiba zingine. Ninaomba sana na kuwasihi ndugu zangu, kaka zangu, wakubwa zangu, Waheshimiwa Wabunge, tumeelewana? Kwa hiyo, hakuna kosa lolote lililofanyika. *(Makofi)*

Hivi kweli, mimi ninaweza kukosea, Katibu wa Bunge atakosea? Mwanasheria wa Bunge atakosea? Makatibu Mezani watakosea? Hawawezi. Nendeni kwenye mitandao tazameni Wabunge wanavyoapishwa kwenye Mabunge yote ya Jumuiya ya Madola. Bunge la Malawi, Spika anakaa; wewe unaapa, Spika amekaa.

Kwa hiyo, leo nitasimama, nitakaa, ndiyo utaratibu ulivyo. Sasa hii ni taarifa rasmi, Waheshimiwa Wabunge mfahamu, na vilevile, wananchi ambao nao walikuwa wanahoji wajue ni utaratibu ambao uko katika kanuni zetu. Nitawasomea ili na wananchi vilevile ambao ni wadau wetu wakubwa waweze kujua.

Mamlaka ya Spika; katika kutekeleza majukumu yake yaliyotajwa katika Ibara ya 84 ya Katiba Spika ataongozwa na Kanuni na pale ambapo Kanuni hazikutoa mwongozo, Spika anafanya kazi kwa kuzingatia Katiba, Sheria nyingine za nchi, Kanuni nyingine zilizopo, uamuzi wa awali ya Maspika wa Bunge, pamoja na mila na desturi za mabunge mengine yenye utaratibu wa Kibunge unaofanana na utaratibu wa Bunge la Tanzania.

Mbunge atatilia nguvu Kanuni zote za Bunge, na Mbunge yeyote anaweza kusimama mahali pake na kumwarifu Spika kuwa Mbunge fulani amekiuka Kanuni. Siyo Spika amekiuka Kanuni, Mbunge alipokiuka Kanuni. Tumeelewana? Huwezi

ukasimama ukamuuliza Spika umekiuka Kanuni. Kwa sababu Kanuni hizi ni zenu ninyi na mwenye mamlaka ya kuzisimamia ni Spika. Spika akikosea anahukumiwa na Katibu wa Bunge. Waheshimiwa Wabunge, tumeelewana? Mbona hamjibu, tumeelewana? Sasa ninafikiri tumeelewana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**KIAPO CHA UAMINIFU NA TAMKO LA AHADI YA UZALENDO**

*(Kiapo cha Uaminifu na Ahadi ya Uzalendo Kinaendelea)*

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

47. Mhe. Amina Iddi Mabrouk
48. Mhe. Amina Mussa Mkumba
49. Mhe. Amjadi Ussi Salum Pondeza
50. Mhe. Mha. Amosy William Maganga
51. Mhe. Amour Seif Abdalla
52. Mhe. Mha. Andrea Mathew Kundo
53. Mhe. Angellah Jasmine Mbelwa Kairuki
54. Mhe. Anna Richard Lupembe
55. Mhe. Anne Kilango Malecela
56. Mhe. Anthony Peter Mavunde
57. Mhe. Boniventura Destery Kiswaga
58. Mhe. Njalu Daudi Silanga
59. Mhe. Daniel Baran Sillo
60. Mhe. David Mwakiposa Kihenzile
61. Mhe. Lulu Guyo Mwacha
62. Mhe. Lucy Thomas Mayenga
63. Mhe. Anton Albert Mwantona
64. Mhe. Arif Suleiman Premji
65. Mhe. Fagason Aron Nkingwa
66. Mhe. Asha Juma Feruz
67. Mhe. Asha Juma Kombo
68. Mhe. Asha Omar Rashid
69. Mhe. Asha Ramadhani Baraka

70. Mhe. Asha Salum Motto
71. Mhe. Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji
72. Mhe. Asia Abdulkarim Halamga
73. Mhe. Asma Ali Mwinyi
74. Mhe. Asya Ali Khamis
75. Mhe. Asya Sharif Omar
76. Mhe. Athumin Omary Mapalilo
77. Mhe. Deogratius John Ndejembi
78. Mhe. Jesca David Kishoa
79. Mhe. Halima Abdallah Bulembo
80. Mhe. Ayoub Mohammed Mahmoud
81. Mhe. Aziza Sleyum Ally
82. Mhe. Bahati Keneth Ndingo
83. Mhe. Azza Hillal Hamad
84. Mhe. Bakari Bakari Shingo
85. Mhe. Baraka Ulimboka Mwamengo
86. Mhe. Bazilio Kapunda Mbwilo
87. Mhe. Benjamin Lukubha Ngayiwa
88. Mhe. Boniphace Mwita Getere
89. Mhe. Dotto Jasson Bahemu
90. Mhe. Bonnah Ladislaus Kamoli
91. Mhe. Catherine Canute Joachim
92. Mhe. Cecilia Daniel Paresso
93. Mhe. Mha. Chacha Mwita Wambura
94. Mhe. Dkt. Charles Jacob Sungura
95. Mhe. Charles Mhando Njama
96. Mhe. Chiku Athman Issa
97. Mhe. Dkt. Christina Christopher Mnzava
98. Mhe. Hawa Subira Mwaifunga
99. Mhe. Christina Solomon Mndeme
100. Mhe. Clayton Revocatus Chipando

**MHE. CLAYTON REVOCATUS CHIPANDO – MBUNGE MTEULE:** Mimi Clayton Revocatus Chipando – Baba Levo, naapa kwamba nitakuwa mwaminifu kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuitumikia kwa moyo wangu wote, na kwamba nitaihifadhi, nitailinda na kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Sheeria iliyowekwa. Ewe Mwenyezi Mungu nisaidie.

Mimi Clayton Revocatus Chipando – Baba Levo, kwa heshima kubwa naahidi…

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Mheshimiwa soma jina lako sahihi.

**MHE. CLAYTON REVOCATUS CHIPANDO – MBUNGE MTEULE:** Mheshimiwa ndio hilo.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Baba Levo sio jina lako rasmi. Anza upya kiapo chako.

100. Mhe. Clayton Revocatus Chipanda
101. Mhe. Condester Michael Sichalwe

**MHE. CONDESTER MUNDI MICHAEL SICHALWE – MBUNGE MTEULE:** Mimi Condester Mundi Michael Sichalwe, naapa kwamba nitakuwa mwaminifu kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuitumikia kwa moyo wangu wote, na kwamba nitaihifadhi, nitailinda na kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Sheeria iliyowekwa. Ewe Mwenyezi Mungu nisaidie.

Mimi Condester Mundi Michael Sichalwe, kwa heshima kubwa ninaahidi mbele ya Bunge Tukufu kuwa, nitakuwa mtiifu na mwaminifu kwa nchi yangu Tanzania na kwamba ninaahidi kuilinda, kuitumikia na kuitetea Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa nguvu zangu zote na moyo wangu wote. Ewe Mwenyezi Mungu nisaidie.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Mheshimiwa Condester unatakiwa kuapa kwa mujibu wa jina ambalo lipo kwenye kiapo. Usiweke jina la Mundi, apa kwa jina ambalo lipo rasmi.

101. Mhe. Condester Michael Sichalwe
102. Mhe. Cornel Lucas Magembe
103. Mhe. Cosmas Mtesigwa Bulala
104. Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro

105. Mhe. Daniel Awack Tlemai
106. Mhe. Daniel Godfrey Chongolo
107. Mhe. David Ernest Silinde
108. Mhe. Dkt. David Mathayo David
109. Mhe. Dennis Lazaro Londo
110. Mhe. Laurent Deogratius Luswetula
111. Mhe. Deus Clement Sangu
112. Mhe. Devotha Daniel Mburarugaba
113. Mhe. Devotha Mathew Minja
114. Mhe. Dickson Nathan Lutevele Villa
115. Mhe. Edward Olelekaita Kisau
116. Mhe. Edibily Kazala Kinyoma
117. Mhe. Edefonce Joackim Canoni
118. Mhe. Edwin Enosy Swalle
119. Mhe. Elibariki Immanuel Kingu
120. Mhe. Dkt. Emanuel Qambaji Nuwas
121. Mhe. Emmanuel John Khambay
122. Mhe. Emmanuel Peter Cherehani
123. Mhe. Mabula Johnson Magangila
124. Mhe. Enock Zadock Koola
125. Mhe. Eric James Shigongo
126. Mhe. Ester Amos Bulaya
127. Mhe. Esther Edwin Malleko
128. Mhe. Esther Lukago Midimu
129. Mhe. Esther Nicholas Matiko
130. Mhe. Exaud Silaoneka Kigahe
131. Mhe. Mha. Ezra John Chiwelesa
132. Mhe. Fadhili Ally Liwaka
133. Mhe. Fadhili Fabian Ngajilo
134. Mhe. Fadhili Sandali Chilombe
135. Mhe. Faraji Buriani Nandala
136. Mhe. Fatma Ally Rembo
137. Mhe. Dkt. Festo John Dugange
138. Mhe. Festo Richard Sanga
139. Mhe. Dkt. Florence George Samizi
140. Mhe. Florent Laurent Kyombo
141. Mhe. George Natany Malima
142. Mhe. Dkt. George Venance Lugomela
143. Mhe. Ghati Zephania Chomete

144. Mhe. Mha. Godfrey Msongwe Kasekenya
145. Mhe. Grace Elias Mkoma
146. Mhe. Haiderali Hussein Gulamali
147. Mhe. Haji Amour Haji
148. Mhe. Halima Iddi Nassor
149. Mhe. Hamad Hassan Chande
150. Mhe. Hamis Mohamed Mwinjuma
151. Mhe. Hamisi Shabani Taletale
152. Mhe. Hamoud Abuu Jumaa
153. Mhe. Happiness Daniel Ngwando
154. Mhe. Haran Nyakisa Sanga
155. Mhe. Hasnain Gulamabbas Dewji
156. Mhe. Hawa Mchafu Chakoma
157. Mhe. Hemed Sumry Haidary
158. Mhe. Henry Charles Kabeho
159. Mhe. Hija Hassan Hija
160. Mhe. Husna Juma Sekiboko
161. Mhe. Ibrahim Mohamed Shayo
162. Mhe. Imamu Mtumwa Vuai
163. Mhe. Innocent Lugha Bashungwa
164. Mhe. Issa Ally Mchungahela
165. Mhe. Omar Issa Kombo
166. Mhe. Jackson Gedion Kiswaga
167. Mhe. Jacquline Chrisant Mzindakaya
168. Mhe. Jacquline Kainja Andrew
169. Mhe. Jacquline Kandidus Ngonyani
170. Mhe. Dkt. Jafar Rajab Seif
171. Mhe. Jafari Wambura Chege
172. Mhe. Jaffar Sanya Jussa

*(Wabunge Waliotajwa Hapo Juu Waliapa Kiapo cha Uaminifu na Tamko la Ahadi ya Uzalendo)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mamlaka ya Kiti naongeza nusu saa. *(Makofi)*

172. Mhe. Jaffar Sanya Jussa
173. Mhe. James Kinyasi Millya
174. Mhe. Jamila Mahmoud Juma

175. Mhe. Janeth Elias Mahawanga
176. Mhe. Janeth Peter Pinda
177. Mhe. Japhael Masanja Lufungija
178. Mhe. Japhet Ngailonga Hasunga
179. Mhe. Jasmine Chesco Ng'umbi
180. Mhe. Dkt. Jasson Samson Rweikiza
181. Mhe. Jesca John Magufuli
182. Mhe. Jesca Yusa Mbogo
183. Mhe. Joel Arthur Nanauka
184. Mhe. Dkt. Johannes Lembulung Lukumay
185. Mhe. John Francisco Nzilanyingi
186. Mhe. John Stephano Luhende
187. Mhe. John John Nchimbi
188. Mhe. Mha. Johnston Johansen Mutasingwa
189. Mhe. Jonas William Mbunda
190. Mhe. Isack Joseph Copriano
191. Mhe. Joseph Enock Tama
192. Mhe. Joseph Zacharius Kamonga
193. Mhe. Josephine Joseph Kapoma
194. Mhe. Josephine Tabitha Chagula
195. Mhe. Prof. Joyce Lazaro Ndalichako
196. Mhe. Judith Salvio Kapinga
197. Mhe. Juliana Daniel Shonza
198. Mhe. Juma Mustafa Kawamba
199. Mhe. Juma Othman Hija
200. Mhe. Dkt. Juma Zuberi Homera
201. Mhe. Jumaa Hamidu Aweso
202. Mhe. Kabula Enock Shitobela
203. Mhe. Kafiti William Kafiti
204. Mhe. Kakulu Burchard Kakulu
205. Mhe. Kangi Alphaxard Lugola

*(Wabunge Waliotajwa Hapo Juu Waliapa Kiapo cha Uaminifu na Tamko la Ahadi ya Uzalendo)*

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Spika, majina ya Waheshimiwa Wabunge watakaoanza kiapo kesho; Mheshimiwa Kaspar Kaspar Mmuya, Mheshimiwa Kassim Hassan Haji, Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani, Mheshimiwa

Kellen Rose Rwakatare, Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, Mheshimiwa Khalfan Issa Mohamed, Mheshimiwa Khalid Mussa Nsekela, Mheshimiwa Khamis Hamad Yussuf na Mheshimiwa Khamis Kassim Ali.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama mlivyoelezwa na Katibu, kesho tutaanza mapema; na panapo majaaliwa tutamaliza Waheshimiwa Wabunge wote kesho, ninafikiri *by* saa saba, saa nane tutakuwa tumeshamaliza.

Ninaahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 2.17 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 12 Novemba 2025, Saa Tatu Asubuhi)*